**Mpango** aagiza mambo manane serikalini kulinda biashara na mapato

UKURASA 3



**Kijana** afariki dunia kwa kunywa pombe ya gongo kupita kiasi

UKURASA 3


Nipashe TESA

Jumanne Julai 6, 2021

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12

Mkoa waja kivingine kukomesha uchafu

Ukurasa 13

Vijana watisha ubunifu kulinda mazingira, kutunza nafasi mijini

Ukurasa 14

Wadau wanapotamani ruzuku ya pedi

TEKNOLOJIA
NA BEATRICE PHILEMON

Ndivyo ujio corona ulivyoiinua VETA hata kuzipiku nchi za Asia

• Ni kupitia kuzalisha mitambo mahiri

UNAPOZUNGUMZIA teknolojia huenda si watu wote wanafahamu maana ya teknolojia, hata hivyo kwa kifupi inamaanisha kutumia sayansi na mbinu mpya katika utendaji wa kazi wa kila siku.

Kwa mfano, zamani watu walikuwa wanatengeneza siagi ya karanga kwa kutumia zana duni. Kwanza kuzikoboa, kuzikaanga, wengine wakitumia kinu kuzitwanga ili kupata unga na pengine kuzichemsha ili kuzalisha siagi.

Teknolojia imebadilia mchakato, zama hizi wanatumia mashine. Hii inamaanisha wameingiza teknolojia katika utengenezaji wa bidhaa hiyo, anasema Mkufunzi Mfawidhi VETA-Morogoro, Fredrick Notley.

Anasema baada ya kuona idadi ya wajasiriamali wanaotaka mashine za kusaga siagi ya karanga inaongezeka, vyuo vya VETA Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, vimebuni mashine ya kisasa ya kusindika na kuongeza thamani bidhaa za karanga ikiwamo ya kubangua karanga, kukaanga na kusaga siagi. Akizungumza na Nipashe, Mkufunzi Mfawidhi VETA-Morogoro, Fredrick Notley, anasema lengo kubwa la kubuni mashine hizi ni kutengeneza ajira na viwanda ili kuunga mkono sera ya Taifa ya Tanzania ya Viwanda.

Mbali na hilo anaongeza: "Tumesikia vilio vya vijana wanaohitimu kwenye vyuo mbalimbali juu ya ukosefu wa ajira ili kuwafumbua macho kuwa kupitia mafunzo ya VETA, ajira si tabu tena, wanaweza kutengeneza mashine za aina mbalimbali wakauza na kujiongezea kipato."

Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 umetoa fursa kwa Chuo cha VETA Pwani na Morogoro kubuni mashine hizi kwa ajili ya wafanyabiashara wa ndani na kwenye jumuisha za ushirikiano ikiwamo ya Afrika Mashariki na ile ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Hii ni mara ya kwanza kubuni mashine hizi kwa sababu hapo awali zilikuwa zinatoka nje ya nchi hasa katika bara la Asia.

"Lakini baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona uliosababisha nchi mbalimbali kufunga mipaka, kujifungua ndani na hata kuzuia usafirishaji wa ndege za abiria sisi VETA tuliona hii ni fursa kibiashara kwa sababu mashine zilikuwa haziji na wafanyabiashara walikuwa wanahangaika kuzipata," anasema Notley. Anaongeza: "Kutokana na changamoto hiyo, sisi tukaona tubuni mashine za usindikaji wa zao hili."

Notley anafafanua kuwa kazi hiyo waliifanya kutokana na vilio vya vikundi vya wajasiriamali, wakiuliza iwapo kuna uwezekano wa kutengeneza mashine za kusindika karanga.

"Wengi waliuliza kupitia simu za mkononi, wengine walikuja kwenye ofisi zetu za Dar es Salaam, Morogoro na Pwani na mpaka sasa mahitaji ya teknolojia ya mashine hizi ni makubwa hapa nchini, lakini wengi wanataka mashine za kusaga siagi ya karanga," anasema.

Kutokana na mahitaji hayo kuwa makubwa wameamua kubuni mashine ambayo inabangua karanga, kuzikaanga, kusaga siagi ya karanga na kufunganya ambavyo thamani yake ni Shilingi milioni 3.2.

Mashine hizi zote zimebuniwa kuanzia mwezi Machi mwaka huu na wamezileta katika maonyesho ya Sabasaba ili wananchi wazione na VETA ipate wahisani watakaotoa fedha zizalishwe na kuingia sokoni kwa ajili ya wananchi anasema Mkufunzi Mfawidhi Notley.

Anaongeza kuwa mpaka sasa VETA inahitaji wahisani wa kuwapa msaada wa fedha ili kufikia kwenye hatua ya soko.

Lengo kuu ni kununua mashine ya kisasa ambayo itawawezesha kutengeneza mashine kwa wingi kwa ajili ya soko na kufundishia wanafunzi vyuoni, anasema Notley.

Ingawa wamefanikiwa kutengeneza mashine hizo, bado wanahitaji nyingine za kuungia vyuma, kukatia mabati, nyingine ni kwa ajili ya kuyakunja, kuyasokota, ya kutobolea vyuma, kukereza vyuma pamoja na ya kukatulia vyuma, zote zikigharimu Shilingi milioni 350.

Kwa upande wa mfumo wa umeme, anasema bado wanahitaji mtambo unaoitwa PCB 'Printing Machine' na kwamba vifaa hivi vitafundishia wanafunzi na kuzalisha bidhaa kwa wingi, anasema.

"Wananchi wanaopenda kutumia mashine ya kubangua karanga wafahamu kuwa ina uwezo wa kubangua kilo 100 za karanga kwa saa wakati mashine ya kukaanga inaweza kukaanga kilo 60 za karanga kwa saa," anasema.

Anasema mashine ya kusaga siagi ya karanga ina uwezo wa kusaga kilo 20 za karanga kwa saa na kuwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo ya kuandaa 'peanut butter.'

Mkufunzi Fredrick Notley, akionyesha mashine ya kusaga siagi ya karanga inavyofanya kazi. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Julai 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580633

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Waziri: Tumewadhibiti majambazi kimyakimya

• **Ni** walioanza kuibuka tena kwa kasi... *Endelea Uk.2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MRADI UMEME WA NYERERE WAWAKOSHA VIONGOZI WASTAAFU**

MARAIS na Mawaziri Wakuu wastaafu jana walitembelea mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa Mwalimu Julius...

**UKURASA WA 7**

**WATOTO WAFARIKI KWA KULA CHAKULA CHENYE SUMU**

WATOTO wawili katika kijiji na kata ya Ikobe, Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita, wamefariki dunia baada ya kula...

**UKURASA WA 7**

**RAIS SAMIA ATEUA BOSI WA UDHIBITI FEDHA HARAMU**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Fatma Ayoub Mwinyimvua Simba kuwa Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti...




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipata maelezo kwa Ofisa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, alipotembelea banda la benki hiyo kabla ya kuzindua rasmi Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yenye kauli mbiu 'Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu' Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ajira zaidi zamwagwa serikalini

• **Sekta** ya Afya yakumbukwa... *Endelea ukurasa 2*



Abiria wakiwa katika basi la mwendokasi (DART) bila ya kuvaa barakoa ili kujikinga na virusi vya corona kutokana na maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya juu ya ugonjwa huo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Siku 100 za Samia zatajwa neema PSSSF, NSSF

UKURASA 2


**MICHEZO** **WASHIKILIA KIBARUA CHA MANARA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Waziri: Tumewadhibiti majambazi kimyakimya

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAKWE

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema Jeshi la Polisi limewanyamazisha majambazi kimya kimya katika maeneo mbalimbali nchini baada ya hivi karibuni walipotaka kuijaribu serikali.

Hivi karibuni lilianza kuibuka wimbi la ujambazi, huku serikali ikiahidi kukabiliana na vitendo hivyo.

Akizungumzia jana na wananchi wa Kata ya Lufu, jimboni kwake Kibakwe, wilayani Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma, Simbachawene alisema hivi karibuni uhalifu ulitokea na kuonekana kama unaongezeka kwa kasi na baadhi ya matukio ya ujambazi yalisikika katika baadhi ya miji ikiwamo Dar es Salaam, Arusha na Mwanza wakidhani kuwa serikali imelegea, hivyo wakawa wanaijaribu.

Alisema operesheni ya kwanza ya kupambana na majambazi hao imefanikiwa kwa ufanisi mkubwa na sasa operesheni ya awamu ya pili tayari imeanza kwa watu wote wanaofikiri kufanya ujambazi ndiyo njia sahihi ya kujipatia kipato.

"Wapo watu wengine wanafikiri uhalifu utawasaidia, kwa wale ambao wanavichwa vigumu wanaendelea kuichezea serikali kwa kutokutaka kuacha uhalifu, kuacha ujambazi wa kutumia silaha, wanaopenda kubaka na kunyang'anya," alisema na kuongeza:

"Wanaotumia pikipiki kupora, sisi tumeyaweka makosa hayo kama makosa makubwa, tukimkamata tunamalizana naye kimya kimya, wewe utajua kimya kimya tunamalizana kinamna gani."

Waziri Simbachawene aliwataka Watanzania kufanya kazi halali kwa kuwa fursa zipo nyingi nchini kuliko kufanya uhalifu, ambao utawaletea matatizo makubwa na kamwe hawawezi kufanikiwa kwa kufanya shughuli isiyo halali.

"Nawaomba Watanzania, na leo nazungumzia hapa Lufu, Jimbo la Kibakwe, nataka kauli hii ifike nchi nzima, kwamba uhalifu sio dili, serikali ipo makini, tutadili na wahalifu wote mpaka tone la mwisho, acheni kufanya uhalifu, ukiwa mtu wa kupanga mambo yako utafanikiwa tu, lakini uhalifu hauwezi kukusaidia na hata ukikusaidia leo, ni shimo la kutumbukia baadaye na utaishia huko ndani," alisema Simbachawene.

"Aliongeza kuwa wananchi wanatakiwa kushirikiana na serikali katika kudhibiti uhalifu kwa njia ya ulinzi shirikishi, ambapo kila mwananchi anapaswa kutoa taarifa za uhalifu katika eneo lake ili kudhibiti uhalifu katika maeneo tunayoishi.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (katikati), akizungumza alipotembelea banda la Ushirikiano linalotumiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ajira zaidi zamwagwa serikalini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewaita kazini watumishi wa kada za afya 473, waliochaguliwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa sababu mbalimbali ikiwamo kustaafu, kufariki pamoja na wale walioacha kazi.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari.

"Mtakumbuka kwamba Mei 12, 2021 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa taarifa kwa umma ya kupata kibali cha ajira mbadala za kada mbalimbali za afya kutoka Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora).

"Nafasi hizi za ajira na mgawanyo wa kada mbalimbali zilizotokana na watumishi kukoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kama vile kuacha kazi, kufariki na kustaafu," alisema Prof. Makubi.

Alisema nafasi hizo 473, zilitangazwa kwenye Tovuti ya Wizara kuanzia Mei 12, 2021 na kufungwa Mei 25, 2021 na jumla ya maombi yaliyopokelewa kwenye mfumo yalikuwa 19,757 na kati ya hayo waombaji 4,760 hawakukamilisha ujazaji wa fomu hadi hatua ya mwisho.

Alisema kutokana na hali hiyo maombi yaliyofanyiwa uchambuzi ni 14,997.

"Baada ya uchambuzi kufanyika jumla ya maombi 9,338 yalikidhi vigezo vya kuajiriwa kutokana na tangazo letu. Aidha ili kuwapata waombaji wa kujaza nafasi zinazohitajika vigezo vya ziada vilitumika," alisema.

Alisema moja ya vigezo vya kupata nafasi hizo ilikuwa ni wenye ulemavu, waliohitimu elimu zao mwaka 2018 na kurudi nyuma, wenye ajira za mikataba ya muda, pamoja na wenye umri chini ya miaka 45.

Aidha, alisema baada ya uchambuzi kufanyika jumla ya waombaji 473, waliohitajika wamechaguliwa.

Pia, alisema watumishi hao wamepangwa maeneo yenye uhitaji na upungufu mkubwa wa watumishi.

Prof. Makubi aliwataka waombaji wa ajira zinazotangazwa kuwa makini wakati wanapowasilisha maombi ya kazi.

# Siku 100 za Samia neema PSSSF, NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema katika siku 100 za utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, kumekuwapo na mafanikio makubwa ya kiutendaji ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Shirika la Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Waziri aliyasema hayo jana alipotembelea banda la Ushirikiano linalotumiwa na mifuko hiyo kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Julius Nyerere maarufu Sabasaba, kujionea jinsi wanachama na wastaafu wanavyohudumiwa.

"Ninajisikia furaha kama waziri ninayesimamia mifuko hii, katika siku hizi 100 za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kiasi cha shilingi bilioni 100 zimetolewa ili kuwalipa wastaafu na mfuko unaoendelea kulimaliza deni lililokuwapo huku NSSF nayo ikifanya vizuri kwa kuongeza makusanyo ya michango ya wanachama inayofikia Sh. bilioni 100 kwa mwezi," alisema Waziri Mhagama.

Alisema serikali iliwaagiza watendaji wa mifuko yote miwili kufanya tathmini ya kiutendaji ili kutengeneza mfumo endelevu ambao hautatengeneza tena vurugu wala hautasumbua sekta kiujumla na kusumbua wastaafu.

"Nafurahi kuwaambia kwamba tathmini imeshafanyika na sasa wataalamu wanapitia ili kutoa matokeo ya hiyo tathmini na muda si mrefu kazi ikikamilika tutashirikiana na vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri ili kutoa tafsiri ya hiyo tathmini ili tupate ustawi wa sekta kwa ujumla." alifafanua.

Alisema Rais alimemsifu Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, ambaye kwa kipindi kifupi tangu aanze kuuongoza Mfuko huo, umeweza kufanya maajabu kwa kukusanya michango kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa mwezi.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema, ushirikiano wao wa kutumia banda moja ili kutoa huduma, kumewarahisishia wanachama na wastaafu wa mifuko yote miwili kuwasaidia kurahisisha utoaji huduma kwenye eneo moja na kwa urahisi.

"Toka mfuko uanze mwaka 2018 hadi Juni 30, 2021 jumla yawanufaika (wastaafu) 144,000 wamelipwa mafao na tunalipa pensheni ya kila mwezi shilingi bilioni 58 kwa mwezi na tunalipa tarehe 25 ya kila mwezi na hatujawahi kuchelewa, hivyo tunakwenda vizuri, napenda Watanzania waelewe hivyo." alifafanua Kashimba.

Naye Mshomba alisema ukuaji wa mfuko umekua kwa kasi sana katika miaka michache iliyopita mfuko ulikuwa na thamani ya Sh. trilioni 3, lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni kwa mujibu wa hesabu ambazo bado hazijakaguliwa, kuna takribani Sh. trilioni 5.2.

# Mpango aagiza mambo manane

**Christina Mwakangale na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameagiza mambo manane yatekelezwe ndani ya mfumo wa serikali, anayoyaeleza kwamba yatafufua uchumi, biashara na mapato ya nchi, wakizingatia uaminifu.

Pia ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na mifumo mingine ya inayoshirikiana nayo kusimamia mapatoya kodi, kufuta mara moja aina zote za kodi na ushuru zenye mwelekeo wa kukwamisha biashara nchini.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara Kimataifa, Dar es Salaam (Sabasaba), jana jioni, huku akihimiza, taasisi zote za kiserikali kuingia ubia wa kirafiki na wadau wao sekta binafsi.

"Serikali haitavumilia atakayekwamisha biashara na uwekezaji, viwanda vya ndani na kati ili kukua," aliagiza.

Alitaja hatua inayoendelea serikalini hivi sasa, ni kwamba iko mbioni kupitia mfumo mpya wa mapato utakaochochea mauzo ya bidhaa za ndani, tozo na faini zenye kero ziondolewe mara moja.

Kwa mujibu wa Makamu wa Rais, orodha ya maeneo hayo aliyoyaagiza yanajumuisha; kampuni kuwezeshwa kujitambulisha; kutangaza bidhaa na huduma zao sokoni; kukutanisha wazalishaji na wateja; mbinu za ushindani; na mwenendo wa soko na uuzaji.

Zingine alizitaja ni umuhimu wa wazalishaji kujua uhalisia wa soko la ndani na nje ya nchi; kuzingatia mahitaji ya soko na walaji; pia ubora, bei na muda

Alivitaka viwanda viongeze ubora wa bidhaa za matumizi ya ndani katika azma ya kujitosheleza nchini, akitoa mfano bidhaa za chakula na ujenzi.

Aliziagiza wizara na halmashauri zote kujenga uwezo wa wafanyabiashara pia ziweke utaratibu wa kutoa taarifa za mauzo katika maeneo yao.

Kuhusu masoko ya nje, aliielekeza TRA na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kushirikiana kutafuta masoko ya kigeni.

Pia Dk. Mpango aliyerejea juzi kutoka Ufaransa kwenye mkutano wa kimataifa, akihimiza mamlaka za kiserikali kutumia vyema fursa za biashara kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Aliipongeza Benki ya NBC kwa kuwa mdhamini mkuu wa maonyesho hayo.

Alipotembelea banda la NBC, alitoa wito kwa taasisi za kifedha ikiwa ni pamoja na Benki ya NBC kukaa pamoja kama wadau wa sekta na kutafuta namna za kupunguza kiwango cha riba, ili watu wengi zaidi waweze kufaidika na mkopo na kukuza mitaji yao ya biashara.

Aidha, aliishukuru benki hiyo kwa kuwa moja ya taasisi kinara zinazochochea ukuaji wa uchumi nchini na kuwashauri kuendelea kuboresha huduma zao zaidi.

# Mradi wa umeme wa Nyerere wawakosha viongozi wastaafu

**Na Idda Mushi,** RUFIJI

MARAIS na Mawaziri Wakuu wastaafu jana walitembelea mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa Mwalimu Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, na kupongeza jitihada zilizofanywa na Hayati Rais Dk. John Magufuli na Rais wa sasa, Samia Suluhu Hassan kuuanzisha na kuendelea kuusimamia mradi huo.

Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete, alipongeza yaliyofanyika kwenye mradi huo ikiwamo jitihada za kudhibiti athari za mazingira zilizoanza kujitokeza na zitakazojitokeza kwa kuwa mradi wowote mkubwa au mdogo ni lazima uwe na athari.

Alisema akiwa Waziri alihusika pia na ujenzi wa miradi ya kuzalisha umeme miwili (Power Station) ikiwemo Pangani na Kihansi, lakini haikuwa mikubwa kama ulivyo wa Julius Nyerere, huku akiwataka Watanzania kuthamini na kuutunza mradi huo ukikamilika.

Aidha, alipongeza jitihada zinazofanywa na makandarasi kubuni michoro, kusimamia na kujenga mradi huo sambamba na Hayati Magufuli kwa kuchukua uamuzi wa kutafuta fedha na kuujenga kwa kutumia fedha za ndani, hivyo kutimiza ndoto za Hayati Nyerere.

Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, alisema alichokiona kikifanyika katika mradi huo ni kama miujiza, kwani siyo rahisi kufikiri hayo yanayoendelea kufanywa na vijana wasomi wa Kitanzania,na kwamba tukio hilo ni kubwa na la kihistoria.

Mawaziri Wakuu wastaafu waliotembelea mradi huo John Malecela, Cleopa Msuya na Mizengo Pinda walipongeza hatua mbalimbali zilizofikiwa.

Punda alishauri ushirikishwaji wa wadau wengine ikiwamo miradi ya iliyokuwa Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA) na SAGCOT, ili shughuli za kilimo ziweze kufanyika hasa katika bonde na wananchi washirikishwe katika utunzaji wa mazingira , vyanzo vya maji na kuwalinda wanyama kwa manufaa ya mradi.

Malecela alisema mradi huo ni tunu kwa taifa, hivyo baada ya kukamilika unatarajiwa kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, utalii hivyo wananchi wanatakiwa kujivunia sana uwepo wake.

Msuya alisema mradi huo uzingatie pia masuala mbalimbali ya kufanikisha kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji ili kwenda sambamba na mradi huo wa umeme.

Awali, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema ujenzi huo unakwenda vizuri na umekamilika kwa asilimia 54.3, na kuwaondoa hofu Watanzania kuwa mradi huo utakamilika kwa wakati na kuanza kutumika rasmi Juni mwakani.

# Afariki kwa kunywa gongo

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKAZI wa Kijiji cha Kivukoni Kata ya Chiwale, wilayani Masasi mkoani Mtwara, Ally Chihonda (35), amefariki dunia kwa kudaiwa kunywa pombe ya kienyeji aina ya gongo kupita kiasi akiwa katika mkesha wa sherehe za unyago.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kivukoni, Mohamedi Kazibule, alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku, wakati wa sherehe za mkesha wa unyago wa kuwatoa watoto waliokuwa wamewekwa jandoni takribani mwezi mmoja sasa.

Alisema Chihinda tangu Julai 02, alikuwa anakunywa pombe kabla ya sherehe hizo kijijini humo na vijiji vya jirani alionekena muda wote akiwa amelewa baada ya kuungana na wenzake kupita kwenye vigenge vya pombe kwa ajili ya kunywa.

Kazibule alisema alitoka nyumbani kwake mapema asubuhi huku akiaga familia yake kwa kueleza kuwa sherehe za mkesha wowote ule haziwezi kuwa na furaha bila ya kunywa pombe na kulewa, kwani kufanya hivyo ndiyo furaha za mkesha na sherehe zozote zile.

Alisema marehemu baada ya hapo alipita katika kila kigenge kinachouza pombe za kienyeji na kuagiza kisha kuanza kunywa ovyo, huku akieleza kwamba siku ya kufurahi kwa sababu watoto walioko unyago wanatoka, hivyo lazima wawaone wazazi, ndugu na jamaa akiwa wamelewa.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kivukoni, Maulidi Dadi, alisema marehemu alikuwa anakunywa pombe kupita kiasi bila ya kula chakula kutwa nzima jambo lililomsababishia umauti wake.

Alisema kuwa baada ya kuendelea kunywa pombe hizo kwa muda wote ilipofika saa mbili hadi tatu usiku wakati sherehe hizo zikiwa zinaendelea alianguka ghafla na kupoteza fahamu.

Dadi alisema ndugu, jamaa na marafiki walimchukua na kumkimbiza katika kituo cha afya cha Kata ya Chiwale na walipofika hapo kwa ajili ya matibabu hata hivyo walielezwa na mganga wa kituo hicho kuwa kijana huyo tayari ameshapoteza maisha.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya ya Masasi, Miriam Cheche, alisema alipopelekwa katika kituo hicho alishafariki na alipofanyiwa vipimo vya kitabibu na daktari wa zamu vilionyesha alikuwa amekunywa pombe kupita kiasi bila kula chakula.


**ZABUNI YA UANDAAJI WA VITALU/BUSTANI ZA MITI**

Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) ni asasi ya kiraia inayofanya shughuli za ulinzi na uhifadhi wa mazingira na rasilimali za maliasili nchini Tanzania. LEAT kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo Endelevu Rukwa (RUSUDEO) lililopo Manispaa ya Sumbawanga na kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) inatekeleza mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili katika Halmashauri za Sumbawanga and Nkasi. Mradi huu unalenga kuongeza uelewa wa jamii juu ya usimamizi endelevu wa maliasili huku mkazo ukiwekwa katika usimamizi wa rasilimali za misitu, wanyamapori, maji, na ardhi. Mradi huu ni wa miaka mitano (5) ulianza Machi 6, 2020 hadi Machi 5, 2025 unaotekelezwa katika kata sita na vijiji 15.

Katika kuwezesha jamii kulinda na kuhifadhi misitu, ardhi, wanyamapori na vyanzo vya maji na kudhibiti mabadiliko ya tabianchi, LEAT inadhamiria kushirikiana na vijiji kupanda miti kwenye kaya na maeneo ya umma (kama misitu na vyanzo vya maji) ili kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kutokea kwa kasi. Hivyo, LEAT inatafuta mtu binafsi, asasi ya kiraia au kampuni yenye uwezo wa kuzalisha miche mbalimbali ya uhifadhi na kurejesha uoto wa asili, kivuli, uchumi na matunda na kuigawa kwa wananchi wa kata za Mwadui, Kalumbaleza na Muze (wilaya ya Sumbawanga) na Kipande, Nkandasi na Mkwamba (Wilaya ya Nkasi).

**Sifa za Mwombaji**

1. Mwombaji awe na uwezo wa kuanzisha bustani za miti (nursery) katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa yaani Kata ya Kipande, Nkandasi na Mkwamba (Wilaya ya Nkasi) na Kata ya Muze, Kalumbaleza na Mwadui (Wilaya ya Sumbawanga); na
2. Mwombaji awe na historia ya kuzalisha miti angalau elfu hamsini.

**Miche ya miti itakayozalishwa:**

| Miche ya miti kurejesha uoto wa asili | Miche ya miti yenye kulinda vyanzo vya maji | Miche ya miti kwa ajili ya uchumi (mbao) | Miche ya miti ya matunda (jamii ya michungwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 150,000 | 90,000 | 45,000 | 7,000 | 292,000 |

Mwombaji atume: (1) barua ya maombi, (2) maelezo juu ya namna atakavyoendesha kazi, (3) nyaraka za usajili wa taasisi, na (4) maelezo ya wasifu binafsi na uzoefu juu ya kazi zilizopita na mawasiliano ya watu aliowahi kuwapa huduma.

Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 19 Julai 2021.**

**Maombi yote yatumwe kwenda kwa:**

**Chief of Party (COP)**
**Lawyers' Environmental Action (LEAT)**
**Jengo la Mazingira, Mtaa wa Mazingira**
**Mikocheni "B", S.L.P 12605, Dar es Salaam.**
**Au kupitia baruapepe: info@leat.or.tz**

116345402

RIPOTI MAALUM -2

USUGU SHIDA YA AJIRA

# Tatizo lilivyokuwa mtihani zama za Mwinyi, Mkapa

• Mkapa alilia na wazazi; Samia aanika hali ya leo

Na Sanula Athanas

***BAADA ya kupata simulizi ya awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi, mfumo wa ajira na misukosuko yake, kwa kiasi kikubwa katika mfumo hodhi wa uchumi hadi kukoma kwa miaka 24 ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, Tanzania mpya na mfumo huria wa uchumi na ajira zake zikachukua nafasi. Endelea...***



Rais Samia Suluhu Hassan akinyanyua juu Kitabu cha Historia ya Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, baada ya kukizindua katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Convention Centre jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA**

**MZEE RUKHSA**

Kuingia kwa awamu ya pili ya uongozi wa nchi kuliendana na kuibuka mpasuko mkubwa wa fursa za uongozi na ajira hasa kwa wasomi ambazo wakati huo zilikuwa za uhakika.

Viwanda vilivyoanzishwa na kampuni lukuki havikuweza tena kumudu ushindani wa soko duniani, ambako pia nchi za mashariki zilizokuwa na soko hodhi, zilianza kuelemewa kimataifa na wenzao wa magharibi.

Soko huria rasmi likatua moja kwa moja nchini na kilio ghafla kikahamia kwa mashirika ya umma, maarufu 'SU', ambayo katika namna hiyo hiyo, yakawa mzigo kwa serikali.

Sababu kubwa ni 'SU' kushindwa kumudu ushindani na pato la serikali likawa duni. Hata kihistoria wasomi na wafanyabiashara wa Kitanzania walikuwa wageni katika soko huria.

Hapo ndipo penye mzizi wa hoja ya Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', katika kipengele anachotaja sababu zilizomsukuma kubinafsisha mashirika ya umma.

Ikumbukwe mashirika ya umma nchini yamekuwapo kisheria tangu mwaka 1969, ikiwa ni muda mfupi baada ya Azimio la Arusha la mwaka 1967. Mzee Mwinyi analalamika ubinafsishaji huo wa mashirika ya umma ulilazimika kufanyika kutokana na taasisi hizo kugeuka waomba msaada serikalini badala ya kurejesha faida.

Mbali na kuelemewa kwake, Mzee Mwinyi anataja kadhia za uzembe, rushwa, ubadhirifu, uwezo mdogo kimenejimenti na uzoefu duni wa kulinda mali zake, ni sehemu ya orodha ya yaliyomsukuma kubinafsisha 'SU', msamiati uliobatizwa jina la mtaani la 'Soma Ule' kutokana na uhalisia wa kusimamiwa na wasomi.

Mzee Mwinyi anaendeleza simulizi yake: "Baada ya Azimio la Arusha, tulitaifisha kampuni, biashara na huduma binafsi, zikiwamo shule na huduma za afya, serikali ikiwekeza zaidi kwenye kuanzisha mashirika mapya ya umma.

"Mwalimu Nyerere na sisi sote tuliamini kuwa mashirika haya yatazalisha faida kubwa maana tangu hapo walikuwa na ukiritimba wa bidhaa na biashara."

Anarejea ushuhuda wa uongozi wake kwamba kilichotokea kwenye mashirika hayo ni utekelezaji duni ambao haukuleta matumaini na mafanikio kutokana na ushahidi uliokuwapo kinadharia.

"Mashirika yalijiingiza kwenye gharama zisizohusika na kazi zao za msingi na kuchangia kuongeza hasara. Mfano, mashirika yaliajiri wafanyakazi wengi kuliko mahitaji halisi.

"Ilikuwa kama mashindano kila shirika kuwa na hospitali yake, idara yake ya usafiri na vikundi vya michezo na utamaduni. "Ripoti ya Shirika la Ukaguzi la Tanzania 1992/93, ilibainisha kwamba kwa ujumla wao (mashirika ya umma) waliitia serikali hasara ya Sh. bilioni 46 kwa mwaka mmoja tu.

**AWANYIMA WASOMI AJIRA**

Mzee Mwinyi anabainisha kuwa uhaba wa ajira kwa wasomi wa elimu ya juu nchini ulianza kujitokeza mwishoni mwa awamu ya kwanza ya utawala wake.

Anakumbusha kuwa kwa mara kwanza mwaka wa fedha 1989/90, serikali ililazimika kutokuwaajiri wahitimu wote wa vyuo vikuu kutokana na hali mbaya ya kiuchumi. Kabla ya hapo, wahitimu wote walikuwa wanaajiriwa.

**JEDWALI LA SENSA TANZANIA**

| Mwaka | Idadi ya Watu | Tanzania Bara | Zanzibar |
|---|---|---|---|
| 1967 | 12,313,469 | 11,958,654 | 354,815 |
| 1978 | 17,512,610 | 17,512,610 | 476,111 |
| 1988 | 23,095,878 | 22,455,193 | 640,685 |
| 2002 | 34,569,232 | 33,584,607 | 984,625 |
| 2012 | 44,928,923 | 43,625,354 | 1,303,569 |

**Matokeo ya sensa zilizopita za watu na makazi nchini.**
**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Juni 7, 2021.**

"Kwa mara ya kwanza serikali ikasema haitaajiri kila anayemaliza masomo ya chuo kikuu, isipokuwa kwa sekta kama afya, elimu na taaluma kama vile wahandisi na wahasibu. Mwaka huo, kati ya wahitimu 552, tuliajiri 99 tu," Mzee Mwinyi anabainisha.

Hatua zingine zilizochukuliwa kwa mujibu wa kitabu chake hicho, ni pamoja na serikali yake kuwapunguza wafanyakazi 310 wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) lililokuwa linasuasua, huku ofisi zake sita nchini na ughaibuni zikifungwa.

**ZAMA ZA MKAPA**

Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, hakuwa mbali katika kuunyoshea kidole uhaba wa ajira nchini, lakini anatofautiana na mtangulizi wake katika eneo analozama kwenye falsafa ya tatizo.

Hata hivyo, miundombinu, mfumo na mazingira ya uchumi ni yaleyale aliyoyarithi kutoka kwa mtangulizi wake.

Katika sura ya mikakati yake ya maboresho ya uchumi, moja ya ajenda kuu za Mkapa ilikuwa ni kukabili mfumuko wa bei ambao kwa wakati huo ulizidi asilimia 20.

Hatua hiyo ilijumuisha kubana matumizi kulikoendana na kusitisha ajira mpya kwa wastani wa nusu ya awamu ya kwanza ya uongozi wake, sambamba na kupunguza majukumu na miundombinu ya kiserikali aliyohisi kuwa sehemu ya mizigo, mojawapo kuuza nyumba za watumishi wa serikali.

Wakati Mzee Rukhsa anaoanisha kukua kwa rasilimali na gharama ya uendeshaji ndiyo tatizo, mrithi wake Rais Mkapa aliyejikita katika kaulimbiu 'mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe', alizama katika falsafa kwamba uhaba wa ajira unaumizwa zaidi na idadi ya watu.

Katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Kusudio la Maisha Yangu), Mkapa anasisitiza ongezeko la watu ni tishio kwa maendeleo ya nchi na kushauri kuwe na mjadala wa kisera kulikabili.

"Ongezeko la watu katika nchi siyo kipimo cha maendeleo, bali ni kikwazo kwa maendeleo. Shida kubwa ya nchi nyingi za Kiafrika hatuna mjadala madhubuti kuhusu sera ya idadi ya watu katika nchi zetu," Mkapa analalamika.

Anagusia ubashiri wa kisayansi wa mwelekeo wa sensa zijazo kwamba kufikia mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (1999-2025), nchi itakuwa na wakazi milioni 67. Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 947,300.

Katika kitabu chake hicho, Mkapa anabainisha kuwa wakati wa uhuru mwaka 1961, kulikadiriwa kuwapo Watanganyika milioni 10.4 na idadi iliongezeka hadi Watanzania milioni 27.4 alipoanza kukalia kiti cha urais mwaka 1995 na iliongezeka hadi milioni 36.1 alipoondoka madarakani mwaka 2005.

Vilevile, Ripoti ya Juni 21, 2017 ya Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) ilibainisha Tanzania imo kwenye orodha ya nchi tisa zinazochangia kasi ya ongezeko la watu duniani, ikitangazwa kuwa ya nne barani Afrika.

Ripoti hiyo inaitaja India, taifa linalokadiriwa kuwa na watu bilioni 1.392 mwaka huu, ndiyo ya kwanza kwa kasi kubwa ya ongezeko la watu. Katika nchi nane zinazofuata, tano ni za barani Afrika. Kati yake, tatu ziko kusini mwa Jangwa la Sahara na mbili ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Orodha ya mataifa hayo kwa nafasi zake nyuma ya India ni: Nigeria; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC); Pakistan; Ethiopia; Tanzania; Uganda na Indonesia.

Kwa kurejea uhalisia wa takwimu za sasa nchini, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inabainisha makadirio ya idadi ya watu nchini hadi mwaka jana (2020) ni 59,441,988.

Mchanganuo huo unaonyesha kuwapo ziada kidogo ya wanawake, waliopo ni 30,309,750 dhidi ya wanaume 29,132,238, ikiwa ni tofauti ya watu 1,177512. Huo ni uwiano wa wastani wa wanawake asilimia 50.99 na wanaume asilimia 49.01.

Akihutubia katika mkutano wake na wanawake jijini Dodoma Juni 8, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alitaja idadi ya Watanzania wenye ajira rasmi kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017 kwamba ni wastani wa milioni tatu (takwimu halisi 3,014,106).


Huo ni wastani wa asilimia tano ya Watanzania kwa mujibu wa takwimu za sasa, ndiyo wako kwenye ajira rasmi.

***Usikose kesho CAG na wadau walioko jikoni wanavyoibua uhalisia uliopo.***

TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**WAKALA YA BARABARA TANZANIA**

# SALAMU ZA RAMBIRAMBI




**Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa TANROADS tumepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Kiongozi na Mpendwa wetu ENG. PATRICK MFUGALE kilichotokea tarehe 29 Juni, 2021 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Jijini Dodoma.**

**Hakika Tutakukumbuka Daima kwa Uongozi wako Mahiri, Uchapakazi uliotukuka, Weledi na Uzalendo wako kwa Taifa Letu.**

**PUMZIKA KWA AMANI MPENDWA WETU.**

www.tanroads.go.tz

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu sahihi chanjo ya Covid-19 itolewe

**JANA** serikali ilitangaza mwongozo kwa shule za msingi, sekondari na vyuo katika kipindi hiki cha corona, na pia imeeleza kuwa chanjo itakuwa bure, huku kukiwa na mikakati ya kuwa na kiwanda cha kutengeneza chanjo hiyo nchini.

Hii ni habari njema kwa kuwa wapo waliokuwa wanahofia gharama za kupata chanjo hiyo, na sasa imepitishwa kuwa ni bure hakutakuwa na gharama zozote.

Uamuzi wa serikali kutoa chanjo hizo bure na kuweka mikakati ya kujenga kiwanda nchini, ambacho kinatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 80 ni wa kupongezwa.

Jitihada hizi za serikali ni za kuungwa mkono kwa kuwa zina kwenda kuhatarisha upatikanaji wa huduma hiyo, ambayo ni hiari kwa kila Mtanzania.

Kumekuwa na taarifa nyingi kuhusiana na chanjo hiyo nchini, ambazo zinaupotoshaji mwingi kiasi cha kuwachanganya wananchi na wengi kuondoa imani juu ya chanjo hiyo na kuanza kuikataa kabla hajaiingia nchini, na hasa kuwapo kwa taarifa za madhara.

Kuna taarifa nyingi ikiwamo muda wa chanjo kuanza kutumika baada ya kutengenezwa, bado haijapitishwa na mamlaka za kimataifa na kuna madhara yaliyoainishwa kwa kila chanjo.

Lakini kuna baadhi ya nchi zimesema aina fulani ya chanjo inayotumika nchi fulani raia wake hawataruhusiwa kuingia nchi za bara fulani, na kutaka chanjo ya nchi fulani kutumika kwa watu wanaotaka kuingia katika nchi hizo.

Ni muhimu elimu kwa umma ikatolewa kikamilifu ili kuondoa upotoshaji mkubwa unaoendelea, kuhakikisha wananchi wanaelewa umuhimu wa chanjo hiyo kwa manufaa yao, kwa kuwa kati ya chanjo zote zipo ambazo ni nzuri na zimethibitishwa na wengi.

Ni muhimu pia kukawa na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma kuhusiana na chanjo, ambazo serikali imeamua kuziingiza nchini baada ya kuridhishwa nazo.

Kwa wale ambao wameshapata chanjo hiyo kwenye mataifa mengine na kuna uthibitisho wake, ni muhimu wakatumika kuelimisha umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ili kuisaidia jamii kuwa na uelewa wa kutosha wa masuala hayo.

Wapo ambao bila kujali taarifa zilizopo wanataka chanjo hiyo, na wenye uwezo wameshaenda nje ya nchi na kuchanjwa na wanaendelea na shughuli zao.

Pia kwa sasa nchi imethibitisha kuna wimbio la tatu la corona, ni muhimu kutoa elimu na kuongeza uangalifu hasa kwenye maeneo yenye mikusanyiko.

Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha mfano kwa kuhakikisha kwenye mkusanyiko wowote anavaa barakoa, hii ikiwa ni kutuma ujumbe kwa umma kuwa lazima wananchi wavae barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.


Bado hatua hazijachukuliwa kwa usafiri wa umma kuhakikisha wananawa mikono muda wote, kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Kwa sasa shule za msingi na sekondari zimefunguliwa na serikali imehuisha mwongozo wa corona uliotolewa mwaka jana, ambao unataka kuwapo maji tiririka na sabuni, uvaaji wa barakoa na kuchukua hatua za haraka kwa wanaoonekana kuugua.

Ni muhimu utaratibu wa kunawa na kuvaa barakoa kwa wanafunzi kutegemea na umri na taratibu za kiafya, kufanya hivyo kwa usahihi ili kusaidia Watanzania kujikinga na ugonjwa huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Makondakta wasiachwe kukwaza maendeleo elimu

**USAFIRI** kwa wanafunzi wanaoishi maeneo ya mijini umegubikwa na kero nyingi ikiwamo kukataliwa na makondakta hali inayosababisha washindwe kufika shule kwa wakati kwa ajili ya kuwahi vipindi madarasani.

Nauli ya mwanafunzi ni Shilingi 200 kwa kila ruti, lakini wanakataliwa kupanda daladala kwa kuwa nauli yao ni ndogo, hali inayowalazimu waachwe kwenye vituo vya daladala kwa muda mrefu wakisaka usafiri.

Wakati mwingine baadhi yao hulazimika kulipa nauli ya mtu mzima ni Sh. 400 hadi 750 kutegemeana na ruti yenyewe, na hivyo kuvurugiwa bajeti yao ambayo inapangwa nyumbani.

Hali hiyo inaonekana kuwa kama ya kawaida katika Jiji la Dar es Salaam, ingawa ni kero na inachangia kukwamisha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi, kwa kuwa baadhi wanachelewa kuhudhuria vipindi vya masomo.

Wanachelewa kwa kuwa wanakaa muda mrefu kwenye vituo vya daladala wakitafuta usafiri, na pia wanachelewa kufika nyumbani kwa wakati kutokana na tatizo hilo la kuzuiwa kupanda daladala.

Kwa ujumla usafiri kwa wanafunzi jijini Dar es Salaam ni kero ambayo ni vyema ikapatiwa ufumbuzi wa kudumu, kwa kuwa ni ya muda mrefu na imeendelea kuwapo.

Usafiri unavuruga bajeti za wazazi na unachelewesha wanafunzi kufika shule au kurudi nyumbani kwa wakati, kwa sababu tu baadhi ya makondakta hawataki nauli ya Shilingi 200.

Si wote wenye tabia hiyo, lakini baadhi yao wanawaacha vituoni watoto wadogo wa darasa la kwanza bila huruma, au kama atakuwa anasindikizwa na mzazi, kondakta anaweza kumwambia mzazi apande mtoto abaki kituoni.

Hayo ndiyo baadhi ya mazingira ambayo wanafunzi wamekuwa wakiyapitia wanapotafuta elimu hasa kwenye maeneo mbalimbali ya mijini likiwamo jiji la Dar es Salaam.

Ni kweli maisha ya shule ni safari ndefu, lakini makondakta wasiifanye safari hiyo kuwa ngumu zaidi kwa kuzuia wanafunzi wasipande daladala na kufika shuleni au nyumbani kwa wakati.

Ikumbukwe, wapo baadhi ya wazazi ambao huwapa watoto wao pesa ambayo inalingana na kiwango chao cha nauli na hawana zaidi ya hapo kulingana na kipato chao cha kila siku.

Wazazi au walezi wa aina hiyo watoto wao wanapotozwa nauli ya mtu mzima, maana yake wanaweza kujikuta hawana nauli ya kurudi nyumbani na kulazimika kuomba kupanda daladala bure.

Hivyo si vibaya mamlaka husika zikaangalia uwezekano wa kuboresha huduma ya usafiri kwa kuhakikisha wanafunzi hawabughudhiwi wanapohitaji usafiri, kwani wanasumbuliwa.

Si makondakta wote wenye usumbufu, lakini asilimia kubwa wanawasumbua wanafunzi kwa sababu tu kwamba nauli yao ni ndogo, hawajui kuwa wanahitajika kufika shuleni kwa wakati. Mkoa unaweza kubuni mkakati wa kununua mabasi maalum kwa ajili ya wanafunzi wa shule za umma wakawa wanalipa nauli hiyo ya Shilingi 200 ili kupunguzia adha wanayoipata kwenye daladala.

Katika mazingira hayo ya kuzuiwa na makondakta, inawezekana wapo baadhi ya wanafunzi wakorofi wanaotumia mwanya huo kufanya mambo yao na kuchelewa kufika shule au nyumbani, kwa kuwasingizia makondakta.

Wapo baadhi ya wanafunzi ambao si asubuhi wala jioni, huwa wapo vituoni bila sababu za msingi, hata wakiitwa kupanda daladala hawataki, hao wanaweza kuwa wanadanganya kwamba wanachelewa kwa sababu ya kuzuiwa kupanda daladala na kumbe ni uongo.

Nauli ndogo ya wanafunzi isiwe kikwazo cha kufika shuleni kwa wakati, lakini wanafunzi wakorofi wasitumie makatazo ya makondakta kuwa kichaka cha kuchelewa kufika shuleni wakisingizia kuzuiliwa kupanda daladala.

# Watoto 2 wafa kwa chakula chenye sumu, 16 wanusurika

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WATOTO wawili katika kijiji na kata ya Ikobe, Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita, wamefariki dunia baada ya kula chakula kinachodhaniwa kuwa na sumu, huku watu 16 wakinusurika.

Aidha, baba wa kambo anadaiwa kumbaka mwanawe wa kufikia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea Julai 3, mwaka huu, kwa kile kinachoelezwa watu hao walikula kiporo cha wali na nyama kilichobaki wakati wa sherehe Julai mosi, mwaka huu.

Alisema chakula hicho kilitokana na sherehe iliyofanyika nyumbani kwa familia ya Kasongwe Luswigilo.

Alisema familia hiyo iliwaalika wageni mbalimbali kutoka kijijini humo na siku iliyofuata walikula kiporo cha wali na nyama ya kondoo.

"Watu hao walianza kuharisha na kutapika baada ya kula chakula hicho na kisha kukimbizwa katika Kituo cha Afya Iboya wilayani Mbogwe, kwa ajili ya matibabu ambapo wawili wamefariki dunia na waathirika 16 wamenusurika na wanaendelea na matibabu," alisema.

Aliwataja waliofariki ni Manyilizu Joseph (6) na Berita Mateso (5) wote wakazi wa kijiji na kata hiyo.

Kamanda Mwaibambe alisema kuwa Jeshi la Polisi limechukuwa sampuli ya mabaki ya chakula hicho kwa ajili ya uchunguzi zaidi yamepelekwa kwenye Ofisi ya Mkemia Mkuu.

**Wakati huo huo,** Kamanda huyo alisema jeshi hilo linamshikilia Vincent Said (27) mkazi wa kijiji cha Sobola, Kata ya Magenge wilayani Geita kwa tuhuma ya kumbaka mwanafunzi wa darasa la kwanza mwenye umri wa miaka saba.

Alisema mtuhumiwa aliyefanya ukatili huyo ni baba wa kambo wa mwanafunzi huyo.

## Kinamama, watoto wajengewa zahanati

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMPUNI ya Ununuzi wa Tumbaku ya Tanzania (JTI) imetoa Sh. milioni 280, kwa ajili ya ujenzi wa zahanati katika kijiji cha Misayu Kata ya Ubagwe Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, ili kusogeza huduma karibu na wananchi na kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Kijiji hicho kina zaidi ya wakazi 3,000 na tangu nchi ipate uhuru hakijawahi kuwa na zahanati na kinamama walilazimika kujifungulia majumbani na kuhudumiwa na watu wasio na sifa za utabibu.

Meneja miradi wa kampuni hiyo, Oscar Luoga, alisema kampuni hiyo imetoa fedha hizo ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa wakulima kwa kurudisha faida baada ya kununua na kuuza mazao yao.

Alisema wametoa Sh. milioni 465, kati ya hizo Sh. milioni 280 za ujenzi wa zahanati, Sh. milioni 35 za vifaa tiba na Sh. milioni 150 za kujenga mabwawa ya maji ambayo yatawasidia kuondokana na uhaba wa maji nyakati za kiangazi jirani na zahanati hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alisema wataendelea kuzihimiza kampuni zingine zinazonunua tumbaku wilayani hapa kurudisha sehemu ya faida wanazopata kwa wananchi, ili kutatua kero zinazowakabili za afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara.

**Tutaendelea kuzihimiza kampuni zingine zinazonunua tumbaku wilayani hapa kurudisha sehemu ya faida wanazopata kwa wananchi, ili kutatua kero zinazowakabili za afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara.**




Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akipata maelezo ya shughuli za kampuni ya madini ya Barrick kwa ofisa wa kampuni hiyo, Antony Sebastian, alipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya 45 yanayoendelea jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Transfoma za umeme mradi wa Nyerere zawasili

**Na Joseph Mwendapole**

SHEHENA ya kwanza ya transfoma zitakazotumika kuzalisha umeme wa Megawati 2,115 kwenye bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) Rufiji Mkoa wa Pwani imewasili nchini.

Jana Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alishuhudia transfoma sita zilizoshushwa katika Bandari ya Dar es Salaam na kuagiza ziwe zimefika kwenye mradi kabla ya Julai 12.

Dk. Kalemani alisema lengo la ziara yake bandarini ni kuhakikisha taratibu zote za kutoa mzigo wa transforma hizo zinakamilika kwa wakati ili kuwezesha mkandarasi aliyeko katika Mradi wa JNHPP kukamilisha kazi ya ufungaji transforma hizo kwa muda uliopangwa.

Aliwaagiza wataalamu kutoka Wizara ya Nishati kufanya maandalizi ya kutoa mizigo hiyo mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu wa mitambo kukaa muda mrefu bandarini na kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi.



Transfoma 29 ndizo zinazohitajika kwenye mradi, lakini ni sita ambazo zimeshawasili bandarini na kuanza kusafirishwa kuelekea eneo la mradi.

Dk. Kalemani alisema shehena nyingine inatarajiwa kuwasili Julai 15, 2021, Agosti 15, 2021 na Septemba 15, 2021.

Alisema serikali imeshatuma wataalamu nje ya nchi kukagua mitambo mingine ya kuzalisha umeme (turbines) ili kujiridhisha kama inatengenezwa kwa viwango kulingana na mahitaji.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Mei, 2022 utakuwa ni mwezi wa kufanya majaribio, matayarisho na matengenezo ya kufunga mitambo ya kuzalisha umeme kabla ya uzinduzi rasmi wa mradi huo unaotarajiwa kufanyika Juni, mwakani.

## Rais ateua Kamishna wa FIU

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Fatma Ayoub Mwinyimvua Simba kuwa Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU).

Kabla ya uteuzi huo, Fatma alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMS), Dar es Salaam.

Taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilieleza jana kuwa uteuzi huo ulianza jana.

# Balozi Mulamula awaita wawekezaji kutoka nje

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amewaomba washiriki wa Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) kutoka mataifa mengine kuja kuwekeza nchini.

Balozi Mulamula alitoa wito huo alipotembelea maonyesho hayo yanayoendelea katika viwanja vya Julius Nyerere Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema tofauti na ilivyokuwa mwaka jana, mwaka huu idadi ya washiriki kutoka mataifa mengine nje ya Tanzania imeongezeka.

"Mwaka jana idadi ya washiriki katika maonyesho haya ilikuwa ndogo sana, kutokana na ugonjwa huu (Covid-19), ambao umeikumba dunia, lakini mwaka huu idadi yao imeongezeka sana, na ni jambo la kujivunia na kushukuru sana," alisema.

"Na kikubwa zaidi wamekuja na bidhaa bora sana, na nimewaambia kwamba wasiishie tu kuja kutuonyesha hizo bidhaa zao kwenye kipindi cha maonyesho, ila waje pia kuwekeza nchini wazalishe kabisa hizo bidhaa."

Mulamula alisema kaulimbiu ya mwaka huu ya maonyesho hayo, imeendana na ya wizara hiyo ya kukuza diplomasia ya uchumi, na kwamba malengo ya mkakati wake ni kutetea maslahi ya taifa kiuchumi pamoja na mambo mengine yanayohusu nchi.



Baadhi ya wanachama wa kikundi cha wakulima cha Tujitambue Kijiji cha Bwenda, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakihudumia shamba lao la mihogo juzi, ambalo ni miongoni mwa mashamba darasa yanayotumiwa kujifunza kilimo bora cha zao hilo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wamachinga wawatimua mgambo

**Na Mohab Dominic,** KAHAMA

ASKARI mgambo kadhaa wameonja 'joto la jiwe' baaada ya kutimuliwa na wajasiriamali wa mboga na matunda katika soko lililoko Mtaa wa Majengo Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, John Kitambi, alisema mgambo hao walijikuta wakitumuliwa na wajasiriamali hao baada ya kutaka kuwalazimisha wahamishie bidhaa zao katika soko la ndani.

Kwa mujibu wa maelekezo ya serikali, wajasiriamali hao wanatakiwa kufanyia biashara zao ndani ya soko, hatua ambao wao wanaipinga na kusema kwamba wanataka wafanye biashara zao nje eneo hilo kwa kuwa ndipo kuna wateja wengi.

Mwenyekiti huyo aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari juu ya wajasiriamali hao kubughudhiwa na mgambo wanaodai ni agizo kutoka juu kwamba hata siku mnada wa wajasiriamali wa matunda na mboga wanapaswa kufanya biashara zao ndani ya soko.

Kitambi alifafanua kuwa kila Jumapili ya wiki ni siku ya mnada katika soko hilo, ambao hujumuisha wajasiriamali na wafanyabiashara wengine wanaotoka sehemu, ikiwamo maeneo ya Namanga, Kazaroho na Kagongwa.

"Ni vigumu kuwalazimisha wajasiriamali wote wafanye biashara ndani ya soko la majengo wakati siku hiyo ya gulio watu wameacha masoko huko wamekuja kwenye mikusanyiko ya watu wengi kujitafutia riziki na ikumbukwe ndani ya soko hilo hakuna nafasi, unawapeleka wakazibe nafasi za wahusika na kusababisha ugomvi," alisema Kitambi.

Alisema mgogoro huo umedumu kwa wiki nne na wajasiriamali hao walitaka kufanya maandamano ili kupeleka malalamiko yao kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, ili wasibughudhiwe waachwe wafanye biashara kwa kuwa gulio hilo ni la mara moja kwa wiki.

Alisema mkakati wa Serikali ya Mtaa wa Majengo ni kuhakikisha wanakutana na uongozi wa soko na kuzungumza ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Dickson Deus, aliomba serikali ya wilaya kuingilia kati suala hilo, kwa kuwa wanahitaji kufanya biashara katika mazingira tulivu lakini askari mgambo wanawasumbua.

Mjasiriamali mwingine kwenye soko hilo Seif Moshi, aliomba kutengwa eneo kwa ajili yao ili kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa kama inavyojitokeza sasa.

## Sekta binafsi yapewa unafuu kuchangia WCF

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), umepunguza kiwango cha uchangiaji kwa sekta binafsi kutoka asilimia moja ya awali ya sehemu ya mishahara ya wafanyakazi hadi asilimia 0.6.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Dk. John Mduma, alisema lengo la kupunguza kwa upande wa sekta binafisi ni kuhakikisha wanaipa uhuru sekta hiyo kuendelea kukua kwa kasi katika uchangiaji ajira na uchumi.

"Na hii ni dhana kamili ya utekelezaji wa marekebisho ya kuhakikisha sekta binafisi inakua kwa kasi na kuleta mabadiliko makubwa katika uchumi wa nchi," alisema Dk. Mduma.

Mkuu wa kitengo cha takwimu katika mfuko huo, James Tenga, pamoja na mambo mengine, alisema kupunguza kiwango cha uchangiaji kwa sekta binafsi kutachangia kuboresha pia biashara nchini.

"Pia hii itasaidia kuleta fursa kwa waajiri kuongeza ajira kwa wafanyakazi na kuwaboreshea maslahi yao. Tunawaelimisha wateja wetu kutumia fursa ya punguzo hili," alisema Tenga.

Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini katika mfuko huo, Dk. Msalamu Omary, alisema pia wamekuwa wakifanya tathmini katika masuala ya watu wenye ulemavu kuhakikisha wanapata haki zao.

Alisema miongoni mwa manufaa ambayo mfanyakazi hunufaika ni pamoja kupata fidia anapopata ulemavu wa kudumu akiwa kazini.

# NMB yasaidia ushirika bil. 5/- huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu**

VYAMA vikuu viwili vya ushirika mkoani Tabora vimeingia makubaliano na Benki ya NMB, kutoa huduma za afya.

Benki hiyo inakuwa taasisi ya kwanza kutekeleza mpango wa bima ya afya kwa wakulima.

Kwa kuanzia, imetenga zaidi ya Sh. bilioni 5 kwa ajili ya kuwakopesha wakulima chini ya utaratibu wa ushirika afya.

Utiaji saini wa makubaliano hayo na vyama vya wakulima wa zao la tumbaku yanayohusisha pia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulifanyika mwishoni mwa wiki kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ushirika iliyoazimishwa kitaifa Tabora.

Vyama hivyo ni WETCU na Mirambo vinavyowakilisha vyama vidogo vya wakulima zaidi ya 200 mkoani humo. Kupitia mpango wa Ushirika Afya wanachama wa vyama hivyo wapewa mikopo isiyo na riba na Benki ya NMB kwa ajili ya gharama za matibabu kwa kutumia kadi za NHIF.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alithibitisha kuanza rasmi kutolewa kwa huduma hiyo, baada ya kukabidhi kadi za NHIF wanufaika watatu wa mpango wa Ushirika Afya kwenye kilele cha Siku ya Kimataifa ya Ushirika Jumamosi.

Katika hotuba yake ya kuadhimisha siku hiyo na kabla ya kukabidhi kadi hizo, Waziri Mkuu alizishukuru taasisi za fedha kwa mchango wake wa kuviimarisha vyama vya ushirika na kuvifanya kuwa nguzo muhimu ya kiuchumi.

Kadi za NHIF zilizofadhiliwa na NMB zilizotolewa na Waziri Mkuu kwa wakulima wa tumbaku Kulwa Mfaume, Saleh Mpemba na Athanas Semeduke ni miongoni mwa kadi 102 za kwanza ambazo zimetolewa na benki hiyo na kuifanya kuwa ya kwanza kufanya hivyo.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema wana mpango wa kuongeza kiasi cha pesa kwa ajili ya mikopo ya wakulima ya bima ya afya.

"NMB tumetenga zaidi ya Sh. bilioni 5 kwa ajili ya kukopesha wakulima zaidi ya 300,000 kupata bima ya afya ambayo haina riba kabisa. Kiwango hiki kitaongezeka kutokana na mahitaji na mwitikio wa wakulima," kiongozi huyo alidokeza kabla ya kutiwa saini za makubaliano na vyama vikuu vya tumbaku.

# Ushirikiano Tanzania, Ufaransa ulivyokuza sekta ya kiuchumi

**Na Salome Kitomari**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Joseph Sokoine, amesema urafiki na ushirikiano kati ya Tanzania na Ufaransa umewezesha kukuza sekta mbalimbali nchini na kutoa ajira kwa Watanzania.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya wahitimu 14 wa lugha ya Kifaransa ambao ni wafanyakazi wa wizara hiyo, alisema sekta zilizoguswa na ushirikiano huo ni biashara, uwekezaji, kuimarisha maendeleo ya ushirikiano ikiwamo upatikanaji wa mikopo, utalii na elimu.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Diaspora, Balozi Anitha Mbega, alisema kuanzishwa kwa mfumo wa mashauriano ya kidiplomasia kwa nchi hizo kumesaidia kuwa na mashauriano ya mara kwa mara juu ya wigo mpana wa masuala ya faida ya pamoja kwa pande zote na watu wake.

Alisema licha ya ushirikiano wa muda mrefu lakini Ubalozi huo kupitia kituo chake cha mafunzo cha Alliance De France wamewafundisha lugha hiyo watumishi wa wizara hiyo kiasi cha kuijua na kuwasiliana katika nyanja mbalimbali.

"Ninatarajia tutakuwa na jukwaa la kujadili mambo mbalimbali ya uhusiano wa nchi zetu hizi mbili kwa undani zaidi kwa manufaa ya pande zote. Tanzania itaendelea kufanyakazi kwa karibu na Ufaransa katika kuimarisha na kukuza uhusiano," alisema. Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, alisema nchi 26 Afrika zinazungumza Kifaransa, na kwamba bara hilo ndilo lenye wazungumzaji wengi wa lugha hiyo kwa kuwa mtu mmoja kati ya tisa anazungumza Kifaransa.

Alisema nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), lugha hiyo ni rasmi katika nchi nne, na kwamba uamuzi wa wakuu wa nchi hizo kuikubali lugha hiyo kama moja ya lugha zake rasmi, ni hatua kubwa katika ukuaji wa nchi hizo na itasaidia pia katika utashi wa kukuza uchumi wa kidiplomasia wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Pwaga, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma, jana, wakati alipofanya ziara jimboni humo kuzungumzia masuala mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# Serikali yaruhusu uchimbaji madini Maseyu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI wilayani Morogoro imeruhusu wachimbaji wadogo wanaofanya shughuli za uchimbaji wa madini katika Kijiji cha Maseyu, Kata ya Gwata baada ya kufanikiwa kutatua mgogoro wa umiliki ardhi na leseni ya uchimbaji uliodumu kwa zaidi ya miaka mitano.

Mgogoro huo ulisababisha serikali kusitisha uchimbaji wa dhahabu katika eneo hilo na wachimbaji wadogo zaidi ya 400 kukosa ajira.

Mgogoro huo ulikuwa ukiwahusisha mwekezaji wa madini, Otta Mosha dhidi ya Hamis Lawei, ambaye ni mkulima.

Akizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya, Mwekezaji Mosha alisema kuwa alifika kijijini hapo kwa lengo la kutafiti maeneo yenye madini kwa ajili ya kuanza uchimbani na kuuziwa eneo hilo lenye ukubwa wa hekari 51, mwaka 2011.

Pia alisema baada ya kupatiwa eneo hilo alianza utafiti na kupatiwa leseni ya uchimbaji, lakini akashangaa kuona baadaye baadhi ya wananchi kuvamia eneo hilo na kuanza shughuli za uchimbaji.

"Nilikuja kwa ajili ya utafiti wa maeneo ya kuchimba dhahabu tangu mwaka 2005 na ilipofika 2009 nikapata leseni ya uchimbaji kwasababu nilikuwa nanunua baadhi ya maeneo, lakini hapa nilinunua mwaka 2011 cha kushangaza kabla sijaanza kazi yangu nikakuta kuna mtu kaja anadai ni eneo lake na kuruhusu watu wachimbe," alisema.

Naye Hamis Lawei alisema alinunua eneo hilo kutoka kwa Mwita Maselo, hekari 16 tangu mwaka 2009 na baadaye walijitokeza wachimbaji wengine na kuingia mkataba nao wa kuchimba dhahabu katika eneo hilo.

Baada ya mvutano huo uliodumu kwa muda mrefu, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albart Msando, ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alilazimika kukagua nyaraka zinazomilikiwa na watu hao ili kujiridhisha uhalali wake. DC Msando alisema baada ya kukagua nyaraka hizo alibaini kuwa eneo hilo linamilikiwa kihalali na mzee Hamis na ndugu zake wawili wenye hekari 16, huku mzee Mosha akiwa na leseni halali ya uchimbaji wa madini katika eneo hilo.

Aliwataka wawekezaji hao kuweka makubaliano ya pamoja na kugawana asilimia katika mapato ya uchimbaji huo badala ya kuendelea kuvutana na wananchi wakiendelea kuteseka.

"Nyaraka zenu zinaonyesha kuna mmiliki halali wa eneo na mmiliki wa halali ya leseni, kwa hiyo ili tuendelee kufanyakazi pamoja, inatakiwa kukubaliana kugawana asilimia kila mmoja anufaike na uchimbaji wa eneo hili," aliagiza.

Pia alisema katika ugawaji wa eneo mwekezaji ambaye anachimba madini hayo kwa sasa atachukua asilimia 70 pamoja na uendeshaji wa shughuli zote na mwekezaji mwenye leseni ya uchimbaji atachukua asilimia tano huku mmiliki wa eneo hilo atachukua asilimia 25 ya mapato yote bila kuhusishwa na gharama za uendeshaji.

"Kwa sababu mmiliki wa eneo ni mzee Hassan yeye apate asilimia 25, pia lazima awe sehemu ya wawekezaji ikiwezekana hata kuwa meneja wa eneo hili, pia kwa kuwa mzee Mosha amekubali kuachia eneo apate asilimia tano maana siyo busara kumuacha wakati tutaendelea kutumia leseni yake kwa miaka mitano ijayo," alisema.

Baada ya kufikia makubaliano hayo, Msando aliruhusu kuendelea kwa uchimbaji katika eneo hilo huku akiwataka viongozi wa serikali ya kijiji na kata kuhakikisha sheria zinafuatwa ikiwamo utunzaji wa mazingira na kuwapo kwa huduma za kijamii na za dharura.

HABARI KITAIFA

# Mkakati waja kuongeza uzalishaji pamba

**Na Happy Severine,** SIMIYU

BODI ya Pamba Tanzania (TCB) imezindua kampeni mpya inayolenga kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwa wakulima kutoka kilo 200 kwa hekta hadi 1,000 kwa hekta moja.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jana na Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, katika Kijiji cha Kijereshi Halmashauri ya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Pamba, Marco Mtunga, alisema katika zao la pamba tatizo kubwa siyo bei kama ambavyo wakulima wanasema, bali ni uzalishaji mdogo.

Mtunga alisema wakulima wengi wamekuwa wakitumia nguvu katika kuzalisha badala ya kutumia maarifa na wengi wao wanashindwa kutumia ujuzi badala yake wanatumia nguvu.

Alisema bodi kupitia mkakati huo imejipanga kuhakikisha inabadilisha mfumo wa uendeshaji kilimo hicho kwa wakulima, ambapo katika msimu ujao lengo likiwa ni kufikia uzalishaji wa tani 300,000 kutoka tani 122,000 msimu wa mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ukiruguru, Ereniko Kilembeka, aliwataka wakulima kutumia mbinu mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa na kituo hicho cha Ukiruguru baada ya kuzifanyia utafiti ili kuweza kunufaika na kilimo.

Alisema kuwa katika mkakati huo TARI Ukiruguru imekuja na mbinu mpya ya uzalishaji wa zao hilo kwa kiwango kikubwa, ambayo ni upandaji wa vipimo vya sentimeta 60 kwa 30 ambayo alisema ndiyo itatumiwa na wakulima katika kuongeza uzalishaji.

Naye Mtaalumu wa kilimo cha pamba kutoka Ukiruguru, Dk. Paul Saidia, alimweleza waziri kuwa baadhi ya wakulima katika mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga na Simiyu wameanza kutumia mbinu hiyo mpya ya upandaji kwa vipimo na kuona manufaa yake.

Waziri Mkenda alisema eneo la kuongeza tija, limepewa kipaumbele ambapo maofisa ugani wote nchini hasa kwenye zao la pamba watawezeshwa vifaa mbalimbali ili kuwafikia wakulima wote na kuwapa elimu ya kilimo cha kisasa.




Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) Mkoa wa Shinyanga, wakifunga taa za usalama barabarani katikati ya mji wa Shinyanga.
**PICHA: MARCO MADUHU**

# Wastaafu watarajiwa wapewa mbinu ya kuwaepuka matapeli

**Na Christina Mwakangale**

WASTAAFU watarajiwa wamepewa mbinu za namna ya kuwaepuka watu wenye nia ya kuwatapeli mafao yao, ambayo wamewekeza fedha kwa kipindi kirefu katika sekta ya utumishi wa umma na binafsi.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), James Mlowe, aliyasema hayo kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam, Sabasaba, mwishoni mwa wiki.

Alisema kutokana na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano kati ya matatizo ambayo wanakumbana nayo baadhi ya wanachama wa mfuko huo, ni kutapeliwa.

Mlowe alifafanua kwamba baadhi ya watu ambao hawana nia njema kwa wastaafu hao, hutumia mbinu zao kwa kuanza kutafiti wastaafu waliokaribia kustaafu au wanaosubiria mafao na kuwalaghai kwa kuwatumia ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu ya mkononi.

"Teknolojia imerahisisha maisha, ingawa baadhi wanatumia vibaya na kutapeli wanachama wastaafu, kwamba kuna mafao kwao (hao matapeli) na kuwataka watoe chochote.

"Ifahamike utaratibu wa mfuko kudai malipo nje ya mfumo wetu haupo. Mwanachama atakayekumbana na hili afike ofisini au apige simu na kutoa taarifa kuhusu watu hawa, kusaidia hawa wastaafu wasitapeliwe," alisema Mlowe.

Mlowe alibainisha kwamba mfuko huo uliwakamata watuhumiwa wanne waliohusika na matukio hayo, ambao wengine wapo mahabusu na wengine wamefikishwa mahakamani.

"Tunashirikiana na vyombo mbalimbali kubaini hili, sababu matapeli hawa hutumia mifumo tofauti kufikisha ujumbe kwa wanachama. Wanachama watakaokutana na tatizo hili wawasiliane nasi hata kwa njia ya mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii," alisema Mlowe.

# Stanbic kuchochea elimu bora kwa wote

**Na Mwandushi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imezindua kampeni ya kuchangia madawati 1,000 kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari nchini. Kampeni iitwayo 'STANBIC MADAWATI INITIATIVE.

Kampeni hiyo inayoambatana na kaulimbiu ya "Pamoja Elimu Bora Inawezekana" imelenga kuwahamasisha wadau kutoka sekta mbalimbali kuiunga mkono benki hiyo katika kutengeneza mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi kwa kutatua changamoto ya upungufu wa madawati kwenye shule.

Hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali ikiwamo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako.

Kupitia mpango huo, benki hiyo imeahidi kupanda mti kwa kila dawati litakalochangiwa na Stanbic Tanzania ama wadau wengine ili kuhakikisha mfumo wa ikolojia unatunzwa.

Prof. Joyce Ndalichako alisema serikali inafarijika sana kuona mshikamano uliopo kati ya sekta binafsi na serikali katika kuleta maendeleo jumuishi katika jamii. Pia aliipongeza benki hiyo kwa juhudi zake za kuunga mkono ajenda ya serikali ya kutoa elimu bora kwa Watanzania wote.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja, Omari Mtiga, alisema: "Tunaamini ndoto zote zinawezekana kama tukifanya kazi kwa pamoja. Tutachangia madawati 700 kuelekea lengo na tunawaomba wadau wengine wenye nia njema kutuunga mkono kwa kuchangia madawati 300 kupitia akaunti nambari TZS 9120002466692-STANBIC MADAWATI INITIATIVE, Kwa pamoja, tunaweza kutimiza ndoto za watoto wetu huku tukitengeneza mazingira endelevu kwa ajili ya kesho yao."

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 6, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Wadau wanapotamani ruzuku ya pedi**



Ukurasa 12

Mkoa waja kivingine kukomesha uchafu



Ukurasa 13

Vijana watisha ubunifu kulinda mazingira, kutunza nafasi mijini

TEKNOLOJIA

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Ndivyo ujio corona ulivyoiinua VETA hata kuzipiku nchi za Asia

## • Ni kupitia kuzalisha mitambo mahiri

UNAPOZUNGUMZIA teknolojia huenda si watu wote wanafahamu maana ya teknolojia, hata hivyo kwa kifupi inamaanisha kutumia sayansi na mbinu mpya katika utendaji wa kazi wa kila siku.

Kwa mfano, zamani watu walikuwa wanatengeneza siagi ya karanga kwa kutumia zana duni. Kwanza kuzikoboa, kuzikaanga, wengine wakitumia kinu kuzitwanga ili kupata unga na pengine kuzichemsha ili kuzalisha siagi.

Teknolojia imebadilia mchakato, zama hizi wanatumia mashine. Hii inamaanisha wameingiza teknolojia katika utengenezaji wa bidhaa hiyo, anasema Mkufunzi Mfawidhi VETA-Morogoro, Fredrick Notley.

Anasema baada ya kuona idadi ya wajasiriamali wanaotaka mashine za kusaga siagi ya karanga inaongezeka, vyuo vya VETA Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, vimebuni mashine ya kisasa ya kusindika na kuongeza thamani bidhaa za karanga ikiwamo ya kubangua karanga, kukaanga na kusaga siagi. Akizungumza na Nipashe, Mkufunzi Mfawidhi VETA-Morogoro, Fredrick Notley, anasema lengo kubwa la kubuni mashine hizi ni kutengeneza ajira na viwanda ili kuunga mkono sera ya Taifa ya Tanzania ya Viwanda.

Mbali na hilo anaongeza: "Tumesikia vilio vya vijana wanaohitimu kwenye vyuo mbalimbali juu ya ukosefu wa ajira ili kuwafumbua macho kuwa kupitia mafunzo ya VETA, ajira si tabu tena, wanaweza kutengeneza mashine za aina mbalimbali wakauza na kujiongezea kipato."



Mkufunzi Fredrick Notley, akionyesha mashine ya kusaga siagi ya karanga inavyofanya kazi. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 umetoa fursa kwa Chuo cha VETA Pwani na Morogoro kubuni mashine hizi kwa ajili ya wafanyabiashara wa ndani na kwenye jumuisha za ushirikiano ikiwamo ya Afrika Mashariki na ile ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Hii ni mara ya kwanza kubuni mashine hizi kwa sababu hapo awali zilikuwa zinatoka nje ya nchi hasa katika bara la Asia.

"Lakini baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona uliosababisha nchi mbalimbali kufunga mipaka, kujifungua ndani na hata kuzuia usafirishaji wa ndege za abiria sisi VETA tuliona hii ni fursa kibiashara kwa sababu mashine zilikuwa haziji na wafanyabiashara walikuwa wanahangaika kuzipata," anasema Notley. Anaongeza: "Kutokana na changamoto hiyo, sisi tukaona tubuni mashine za usindikaji wa zao hili."

Notley anafafanua kuwa kazi hiyo waliifanya kutokana na vilio vya vikundi vya wajasiriamali, wakiuliza iwapo kuna uwezekano wa kutengeneza mashine za kusindika karanga.

"Wengi waliuliza kupitia simu za mkononi, wengine walikuja kwenye ofisi zetu za Dar es Salaam, Morogoro na Pwani na mpaka sasa mahitaji ya teknolojia ya mashine hizi ni makubwa hapa nchini, lakini wengi wanataka mashine za kusaga siagi ya karanga," anasema.

Kutokana na mahitaji hayo kuwa makubwa wameamua kubuni mashine ambayo inabangua karanga, kuzikaanga, kusaga siagi ya karanga na kufunganya ambavyo thamani yake ni Shilingi milioni 3.2.

Mashine hizi zote zimebuniwa kuanzia mwezi Machi mwaka huu na wamezileta katika maonyesho ya Sabasaba ili wananchi wazione na VETA ipate wahisani watakaotoa fedha zizalishwe na kuingia sokoni kwa ajili ya wananchi anasema Mkufunzi Mfawidhi Notley.

Anaongeza kuwa mpaka sasa VETA inahitaji wahisani wa kuwapa msaada wa fedha ili kufikia kwenye hatua ya soko.

Lengo kuu ni kununua mashine ya kisasa ambayo itawawezesha kutengeneza mashine kwa wingi kwa ajili ya soko na kufundishia wanafunzi vyuoni, anasema Notley.

Ingawa wamefanikiwa kutengeneza mashine hizo, bado wanahitaji nyingine za kuungia vyuma, kukatia mabati, nyingine ni kwa ajili ya kuyakunja, kuyasokota, ya kutobolea vyuma, kukereza vyuma pamoja na ya kukatulia vyuma, zote zikigharimu Shilingi milioni 350.

Kwa upande wa mfumo wa umeme, anasema bado wanahitaji mtambo unaoitwa PCB 'Printing Machine' na kwamba vifaa hivi vitafundishia wanafunzi na kuzalisha bidhaa kwa wingi, anasema.

"Wananchi wanaopenda kutumia mashine ya kubangua karanga wafahamu kuwa ina uwezo wa kubangua kilo 100 za karanga kwa saa wakati mashine ya kukaanga inaweza kukaanga kilo 60 za karanga kwa saa," anasema.

Anasema mashine ya kusaga siagi ya karanga ina uwezo wa kusaga kilo 20 za karanga kwa saa na kuwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo ya kuandaa 'peanut butter.'

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mkoa waja kivingine kukomesha uchafu




Mhudumu wa afya kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, Ester Luhende, akikusanya takataka kwenye sehemu ya kuzihifadhia iliyoko jirani na ofisi za kata hiyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

VIONGOZI wa taifa hili katika awamu zote hawakusahau kusisitiza usafi wa mtu na mazingira yake. Tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere hadi awamu ya sita usafi unasisitizwa.

Walioshuhudia awamu ya kwanza watazitaja kampeni za Mtu ni Afya kuwa zililenga usafi wa mazingira na wa watu.

Zilihimiza kuwa na choo bora na kukitumia, kuondoa mazalia ya mbu kukwepa malaria, kufyeka vichaka na kufukia madimbwi. Yote ni kuondokana na maradhi

Awamu ya sita ikiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa ni lazima kuhamasisha masuala ya usafi wa mazingira na kutoa maagizo mbalimbali kwa viongozi wa wilaya na mikoa kusimamia.

Kampeni hizo za usafi wa mazingira, zilianzia awamu ya tano, kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kwa kufunga biashara mbalimbali kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 4 usafi unapomalizika.

Kazi ilianzia Dar es Salaam na kusambaa nchi nzima huko wakuu wa mikoa na wilaya wakiisimamia.

Kwa kushirikiana na wakurugenzi wa halmashauri jukumu ni kuhamasisha wananchi kuyatunza mazingira katika maeneo ya biashara, mitaani na katika makazi.

> Mashindano haya pia yataamsha watumishi kila mmoja awajibike sehemu yake kwa kuhakikisha mji unakuwa safi pamoja na kuzolewa taka kwa wakati kwenye maghuba.

**SHINYANGA YABADILIKA**

Machi 2, mwaka huu, Nipashe ilichapisha taarifa za kukithiri uchafu kwenye baadhi ya maeneo Manispaa ya Shinyanga, yenye kichwa cha habari "Nyumba za taka' zilipogeuka adui mkubwa makazi ya watu".

Habari hiyo ilisababisha viongozi wa manispaa hiyo kuchukua hatua kuingilia kati na kusimamia usafi kikamilifu.

Kufuatia hali hiyo ya kukithiri kwa uchafu kwenye baadhi ya maeneo manispaa imezindua mashindano ya usafi wa mazingira, ambapo washindi watapewa zawadi mbalimbali, lengo likiwa ni kuufanya mji kuwa safi.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa Shinyanga, Kuchibanda Snatus, anasema mashindano hayo ya usafi, yanahusu kata zote 17, mitaa 55, vijiji 17 na taasisi zote za umma na za binafsi.

Shule za msingi na sekondari, vyuo, masoko na viwanda na kwamba mashindano hayo yataifanya Shinyanga kuwa safi karibu maeneo yote.

Aidha, ni kukabiliana na magonjwa yatokanayo na uchafu kikiwamo kipindupindu, malaria kutokana na taka, madimbwi kuwa mazalia yake.

Halikadhalika anasema maeneo yatakayokaguliwa kwenye mashindano hayo ya usafi wa mazingira ni kaya zote, shule, masoko, mitaro, barabara, viwanda na maeneo ya wazi.

Pia, utekelezaji wake utasimamiwa na viongozi wa serikali za vijiji, mitaa na kata, kwa kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira kwenye maeneo yote.

**ZAWADI ZA WASHINDI**

"Mshindi wa mashindano haya ngazi ya kaya na shule, atapewa zawadi ya vifaa vya usafi, kiwanda na kata itakayoongoza watapata ngao, mtaa utapata cheti na watakaofanya vibaya watapewa kinyago," anasema Snatus.

"Faida ya mashindano haya ni kuboresha hali ya usafi wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Shinyanga, kupunguza mazalia ya mbu, pamoja na kutokomeza magonjwa yatokanayo na uchafu, ikiwamo kuhara na kipindupindu.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, anasema mpango huo wa mashindano ya usafi wa mazingira, utaondoa kero za uchafu mjini Shinyanga, pamoja kuzolewa uchafu kwenye nyumba za taka kwa wakati, na kuufanya mji huo kuwa safi muda wote.

Anasema mashindano hayo yatakuwa chachu ya kumaliza mrundikano wa taka kwenye nyumba za taka 'maghuba' na kuondoa kero za wananchi kukabiliwa na kuzagaa kwa uchafu mitaani bila sababu.

"Nimekuwa nikizunguka mara kwa mara kuangalia hali ya usafi katika maeneo ya mji hali siyo mbaya sana, ila kuna uchafu mwingi kwenye maghuba hazitolewi kwa wakati, hivyo mashindano haya yatapunguza kwa kiasi kikubwa kero hiyo," anasema Nkulila.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, anasema mashindano hayo yatawajengea uwezo wananchi pamoja na viongozi wa namna bora ya kusimamia masuala ya usafi wa mazingira muda wote.

"Mashindano haya pia yataamsha watumishi kila mmoja awajibike sehemu yake kwa kuhakikisha mji unakuwa safi pamoja na kuzolewa taka kwa wakati kwenye maghuba," anaongeza Mwangulumbi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ni miongoni mwa viongozi ambao wanapigania sana suala la usafi wa mazingira, na hata kulazimika kufanya mikutano ya hadhara kila kata mjini humo.

Pamoja na kutembelea kwenye minada na masoko kuhamasisha wananchi kufanya usafi.

Anasema suala la usafi ni la kila mtu, na halihitaji kuhimizwa sababu ya kulinda afya zao, lakini wao kama viongozi wanajukumu la kuwakumbusha wananchi na kutoa elimu ya utunzaji mazingira, ili watu wabaki kuwa salama na kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

"Sisi viongozi tunawaomba wananchi wazingatie elimu ambayo wanapewa na wataalamu wa afya na viongozi wao, kuhusu kufanya usafi wa mazingira kila mara na siyo lazima mpaka mwisho wa mwezi. Wahakikishe muda wote wanakuwa wasafi," anasema Mboneko.

"Pia waweke vifaa vya kunawa mikono na sabuni na majitiririka kwenye makazi yao, pamoja na maeneo ya biashara zao, ili kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, sababu ugonjwa huu unakabiliwa kwa usafi kuanzia mikono, mazingira ikiwamo kuepuka mikusanyiko," anaongeza Mboneko.

TEKNOLOJIA

**NA CHRISTINA MWAKANGALE**

# Vijana wang'ara ubunifu kulinda mazingira, kutunza nafasi mijini

WAKAZI wa mijini wanaokabiliwa na tatizo la kuishi kwenye vyumba vidogo visivyo na nafasi kubwa za kujaza samani, hawana sababu ya kuhofu tena baada ya VETA kuwatatulia tatizo hilo.

Oswin Komba, mlezi wa kituo cha kulea na kukuza ujuzi wa wahitimu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, (VETA), kwenye fani ya useremala, anasema vijana wabunifu ndiyo wanaomaliza changamoto hiyo.

Komba anasema kituo cha kuatamia wabunifu cha VETA maalumu kwa ajili ya kulea vijana ambao wana mawazo na ubunifu tofauti wa kutengeneza bidhaa za mbao ili kupatikana samani zenye soko kulingana na wakati ni wahusika wakuu.

Anazungumza na Nipashe kuhusu ubunifu wa huo, akisema vijana wamebuni 'meza kitanda tiba', meza kiti cha wapendanao na benchi.

"Ni samani zinazovuta hisia za wanaotembelea Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam."



Oswin Komba, mlezi wa kituo cha kulea na kukuza ujuzi wa wahitimu wa VETA akielezea namna 'meza kitanda tiba' inavyokuwa katika matumizi ya meza na wakati mwingine kutumia kulalia, kwenye viwanja vya Sabasaba. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**MEZA KITANDA TIBA**

Komba anasema kitanda hicho ambacho kimetumia mbao za mitiki, kina matumizi lukuki, kinatunza nafasi na kwamba kinaweza kutumiwa zaidi na vijana wanaoanza maisha, waliopo hosteli ama familia ambazo hazipendi chumba kilichojaa vitu vingi na kwamba kinaokoa nafasi kwa asilimia 75.

"Kwa maisha ya Dar, siyo siri wengi ambao wanaoanza maisha, wanafunzi na vijana hupanga chumba kimoja ambacho ndani yake huwa na vitu vingi na nafasi inakuwa ndogo... sasa kuna ufumbuzi."

"Kabla ya kutengeneza bidhaa tunafanya utafiti mdogo sokoni ndipo tukagundua tatizo hilo. Tukaona tuje na bidhaa za samani kama hizi zinazotunza nafasi ya chumba kimoja na kufanya kuwepo unadhifu."

Anaongeza kuwa kitanda hicho hubadilika kuwa kiti, mchana na usiku kitanda, ukiamka asubuhi unakikunja unaenda kwenye shughuli zako, kwa mujibu wa Komba.

Anasema ubunifu huzingatia mahitaji yaliyopo sokoni, jamii na kwamba hasa vijana waishio mijini na familia zisizo na uwezo wa kukodi vyumba vingi, kutokana na mapato.

Komba anasema kitanda hicho pia ni tiba ya mgongo na kwamba godoro lenye ukubwa mdogo ndilo hutumika, ambalo halibonyei sana likilaliwa.

Pia anasema kitanda hicho kina chaga mbili maalumu ambazo ndani yake zina uwazi kwa ajili ya kuweka mkaa unaosaidia kuvuta hewa ukaa inayozalishwa usiku wakati wa kulala.

"Unapolala chumba kidogo mzunguko wa hewa huwa mdogo. Hili huathiri afya, hivyo mkaa kwenye chaga na kisha ukiweka godoro juu ukilala unapozalisha hewa ya sumu inamezwa na mkaa huo." "Ubunifu huu tuliugundua mwaka jana," anasema Komba na sasa kazi inaendelea."

**SAMANI WAPENDANAO**

Komba anazungumzia kivutio cha meza kiti cha wapendanao akisema kimekuwa na nafasi muhimu kwenye banda la VETA kwa wanaotembelea maonyesho hayo ya Sabasaba.

Anasema samani hiyo ina matumizi tofauti kama dawati la kusomea, meza ya kulia chakula na mapumziko kwa mazungumzo ya wapendanao.

Anasema meza kiti hiyo inapunguza matumizi ya nafasi kwa asilimia 50, ni meza ya bosi katika biashara, mgahawani, dawati shuleni na vyuoni pia inabebeka kirahisi.

"Kiti cha wapendanao sababu kina meza moja iliyobeba viti viwili vilivyoambatana pamoja hivyo hukaa watu wawili tu. Kinatumiwa na baada ya matumizi unakunja na kugeuka meza isiyochukua nafasi kwenye chumba chako," anasema Komba.

**BENCHI KALI**

Komba anazungumzia benchi hilo akisema hugeuka kuwa dawati na kiti cha kupumzikia ambalo mwisho wa matumizi hukunjwa ili kuokoa nafasi kwenye chumba.

Anasema ubunifu wa samani hizi kwa ujumla ulizingatia kuokoa nafasi kwenye chumba au hosteli ambalo vijana na wanafunzi huwa na tatizo la vifaa vya kujisomea.

Aidha ni kupunguza matumizi ya mbao kuzalisha samani nyingi ambao unaweza kuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira

"Tuligundua wanafunzi wa hosteli au bweni katika baadhi ya shule, ukiisha muda wa darasa wakiwa bwenini hawana vifaa vya pamoja au dawati ambalo litaruhusu mjadala wa pamoja.

> Ubunifu wa samani hizi kwa ujumla ulizingatia kuokoa nafasi kwenye chumba au hosteli ambalo vijana na wanafunzi huwa na tatizo la vifaa vya kujisomea.

Benchi hili linachukua watu sita hadi nane kwa wakati moja wakajadili pamoja na wanapomaliza kazi linakunjwa kuwa kiti cha kukalia wageni. "Tuliona wanafunzi hulazimika kubeba madawati ya darasani na kuyaleta bwenini kusomea, bweni hugeuka darasa," anasema Komba.

Benchi hilo lina muundo kama 'vimbwete' madawati ya zege yanayotumiwa na vyuo mbalimbali nchini kwa ajili ya majadiliano na kazi za wanafunzi zinazofanyika nje ya kumbi za mihadhara.

**VIJANA WABUNIFU**

Mkurugenzi Mkuu VETA, Dk. Pancras Bujulu, anasema kuna idadi kubwa ya vijana ambao hawajafika vyuo vikuu ambao ni hazina ya ubunifu na ujuzi.

Anasema vijana hao ambao wengi wao wana elimu ya msingi na sekondari, wanahitaji kufundishwa ufundi stadi ili kujipatia ajira, kukuza uchumi wao na familia zao ikiwamo taifa.

"Mafundi stadi ndiyo wanaendesha moja kwa moja viwanda na shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Tukiwa na mafundi stadi mahiri uzalishaji viwandani utakuwa na tija," anasema Dk. Bujulu.

Anaongeza kuwa walio na elimu isiyofikia chuo kikuu wengi wao wana ujuzi ambao wanaweza kuutumia iwapo watapewa umahiri.

Anafafanua kwamba wapo vijana ambao wamerithi kazi za ufundi kutoka kwa wazazi, walezi au ndugu zao na kufanya kazi vizuri lakini hawatambuliki.

Anasema mafundi hao baada ya kupata mafunzo VETA, watajiajiri na kukuza uchumi na kwamba mafunzo hayo ni mwamko mpya kwa waliokata tama, wanaodhani wamaeshindwa maisha baada ya kushindwa kuendelea na masomo kutokana na changamoto za kiuchumi kwenye familia zao.

Anasema mkakati ni kuwa na vyuo vya VETA katika wilaya zote ifikapo 2025 ili kuhakikisha ujuzi unakua kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa viwanda, akibainisha kwamba matarajio yao ni udahili kuongezeka kutoka wanafunzi 700,000 hadi kufikia milioni moja kwa mwaka.

"Dira yetu ni kuona Tanzania yenye mafundi stadi, mahiri na wa kutosha ili kukuza uchumi." Anasema Mkurugenzi wa VETA

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Wadau wanapotamani ruzuku ya pedi

## • Vijana, kinamama na sasa wasichana

TAULO za kike ni mahitaji muhimu kufanikisha elimu ya wasichana kwa vile kuna baadhi wanaelezwa kuwa wanashindwa kwenda darasani kutokana na kukosa bidhaa hizo za kujisitiri kila mwezi.

Upatikanaji wa taulo hizo ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa kike kuhudhuria kikamilifu na kupata haki msingi ya elimu kama ilivyo kwa wenzao wa kiume.

Vilevile kutokana na umuhimu wa pedi hizo wadau mbalimbali wa elimu wanafanya kampeni za kuhamasisha zipatikane kwa wingi ili kumwezesha mtoto wa kike kuhudhuria vipindi vyote vya masomo bila kukwamishwa.

Hivi karibuni wadau wa elimu, asasi za kiraia, vikundi vya kijamii na wanahabari kutoka mikoa mbalimbali walishiriki katika mafunzo ya siku mbili yaliyolenga kujua umuhimu wa bajeti ya mrengo wa kijinsia ambayo inaweza kutatua changamoto za wanawake zikiwapo pedi.

Mafunzo hayo yanafanyika wakati bajeti kuu ya serikali ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 ambayo ni Shilingi trilioni 36.3, imeshasomwa bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba na kupitishwa.

Katika mafunzo hayo, wadau wanaibua hoja ya kuongeza ruzuku ya wanafunzi inayotolewa na serikali ili ijitosheleze pamoja na kununua mahitaji mengine, iende kwenye manunuzi ya taulo za kike kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wasichana hasa wa kaya maskini.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, wanatoa mapendekezo ambayo wanaamini iwapo yatazingatiwa, yanaweza kusaidia kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa kike kinachokwamishwa na pedi.

Angela Mfinanga ni mwenyekiti wa kituo cha taarifa na maarifa ambacho kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao uliandaa mafunzo hayo, anasema, kuna haja ya kuchukua sehemu ya ruzuku ya wanafunzi kuelekezwa katika manunuzi ya taulo za kike.

"Serikali ianze kutoa maelekezo kwa halmashauri za wilaya kutenga asilimia fulani ya fedha kama inavyotoa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu kusaidia wasichana kupata pedi. Hii iwe ruzuku kwa wanafunzi na ifanikishe kupata mahitaji ya hedhi salama kwa wanaosoma shule ya msingi," anasema Anjela.

Anakiri kwamba, serikali imekuwa ikifanya jitihada nyingi katika kuboresha elimu, lakini anabainisha kuwa katika kumkomboa mtoto wa kike shuleni, bajeti imeendelea kuwa kimya katika upatikanaji wa taulo za kike.

"Hivyo ni vyema ruzuku ya kugharamia elimu ikaongezwa na kuelekezwa kwenye taulo hizo, pia kuwapo na miundombinu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike, walio kwenye elimu ya msingi ili wasiwe na kikwazo kitaaluma," anasema.



Kundi la wadau wanaohitaji rukuzu ya wanafunzi iongezwe ili kununua taulo za kike. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Deogratius Temba, akisisitiza jambo kwa wadau wa taulo za kike

> "Kwa kuwa serikali imepanga kufanya mapitio ya Sera ya Elimu kuendana na muktadha uliopo, binafsi ninaamini na kutarajia ushiriki mpana wa wadau mbalimbali katika mchakato huo muhimu.

### UPUNGUFU KIBAJETI

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Deogratius Temba anasema kuna upungufu wa kijinsia katika bajeti hiyo, kwa kuwa imekaa kimya katika upatikanaji wa taulo za kike na miundombinu ya hedhi salama kwa wanafunzi wasichana.

"Wanafunzi hao ni wa elimu ya elimu ya msingi na sekondari ambao hawapati huduma hiyo kwa sababu bajeti haijataja mafungu au kutoa maelekezo yoyote kwa halmashauri za wilaya au mamlaka za elimu kuzingatia mahitaji ya hayo katika mafungu ya fedha wanayopata," anasema Temba.

Anaongeza kuwa serikali imeendelea kutegemea chanzo kimoja ambacho ni fedha za wahisani kwenye programu ya maji, afya na usafi wa mazingira shuleni (SWASH), huku wasichana na wanawake walioko nje ya shule, wakikosa huduma kwa vile hawawezi kufikiwa.

Mwezeshaji huyo anasema, kwa kawaida bajeti kuu ya serikali hutoa mwelekeo wa mipango ya maendeleo kwa kila sekta kwa mwaka unaohusika, na kwamba bajeti hiyo ni kielelezo cha jinsi gani serikali imejipanga na kupendekeza mwelekeo wa namna afua zilizopendekezwa katika sekta mbalimbali zitagharamiwa ili kuleta mabadiliko kwa mwaka husika.

Temba anafafanua kuwa, bejeti kuu ya serikali ni kielelezo kikubwa na muhimu katika kuashiria jinsi inavyopendekeza kuwaletea wananchi wake maendeleo kulingana na mahitaji au malengo ya kitaifa, lakini kwenye upatikanaji wa pedi hilo halijaguswa.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, wanatoa mapendekezo kadhaa ambayo wanaamini kwamba, iwapo yatazingatiwa, yanaweza kusaidia kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa kike.

### UDAHILI ZAIDI

Mwenyekiti wa kituo cha taarifa na maarifa cha Kiloleli, Kishapu mkoani Shinyanga, Kwangu Limbu, anasema, katika kuboresha elimu kwa watoto wa kike, kuna haja ya kuwapo kwa mafunzo ya ufundi na sayansi.

"Kupitia sekta elimu, VETA na SIDO, ni vyema serikali ikahakikishe mafunzo ya stadi mbalimbali za ufundi na sayansi yanaongeza udahili wa wasichana na vijana wa makundi ya pembezoni," anasema Kwangu.

Anafafanua kuwa, njia hiyo itasaidia kuwafanya wahusika hasa wasichana kuweza kunufaika na ajira zenye tija kuliko ilivyo sasa, ambapo baadhi hujiingiza kwenye mambo hatarishi.

Mdau huyo, anashauri serikali kuendelea kuongeza fursa kwa kila mtoto kwenda shule kwa kugharamia elimu msingi bila ada, ili kupanua wigo kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi wanapata fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari bila vikwazo.

"Kwa kuwa serikali imepanga kufanya mapitio ya Sera ya Elimu kuendana na muktadha uliopo, binafsi ninaamini na kutarajia ushiriki mpana wa wadau mbalimbali katika mchakato huo muhimu," anasema.



## HABARI DODOMA

# Aitaka ndaki UDOM kutambua wabunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NDAKI ya Sayansi ya Asili na Hisabati, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) imetakiwa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu ili wanufaike na bunifu zao mara ya kuhitimu mafunzo hayo.

Hayo yalisemwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Tafiti na Ushauri, Prof. Alexander Makulilo, wakati wa kufunga maonyesho ya wabunifu wa Sayansi wa Ndaki ya Sayansi ya Asili na Hisabati, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Prof. Mabuki alisema ipo haja ya kuwaendeleza wabunifu ili wapatikane wale walio bora zaidi na wafaidike baada ya kuhitimu.

Alisema Sayansi na Utafiti ni mambo muhimu sana katika uchumi wa viwanda, wabunifu wana mchango mkubwa katika kuleta tija kupitia uchumi wa viwanda, hivyo ni wajibu wa serikali kuhakikisha inawasimamia na kuwaendeleza ili kufikia malengo.

"Ni lazima watambuliwe na waendelezwe ili bunifu zao ziwe na tija, bila kutambuliwa wengi wanapotea, nimetembelea maonyesho bunifu nyingi ni nzuri na kama zitaendelezwa zitaleta tija kubwa kwa Taifa," alisema Prof. Makulilo.

Alisema chuo hicho kimeweka mazingira wezeshi katika masuala ya utafiti na bunifu ili kuhakikisha wahitimu wanafaidika na elimu hiyo.

Alisema kupitia Serikali na Wizara ya Elimu wamepata fursa ya Mradi wa High Education Economic Transformation (HEET), Ndaki ya Sayansi itapata maabara kubwa ya kisasa, wataweza kuendeleza utafiti na ubunifu kwa uhakika na kutoa mafunzo ya kufaa ndani na nje ya nchi.

Alisema kupitia mradi huo wanataaluma wana fursa ya kusomeshwa kuanzia mwaka wa fedha unaoanza.

Prof. Makulilo alisema miongoni mwa mikakati ya chuo hicho ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, UDOM inakuwa miongoni mwa vyuo bora 20 barani Afrika.

"Kuna mwanga wa kuelekea huko, tunatekeleza ajenda na malengo makuu ya UDOM, ubunifu ni mkubwa tutafanikisha malengo yetu," alisema.

Naye Mkuu wa Ndaki ya Sayansi ya Asili na Hisabati, Prof Said Vuai, alisema malengo makubwa ya chuo hicho ni kutoa wahitimu ambao watakwenda kutatua matatizo katika jamii.

Alisema ndaki hiyo ilianza mwaka 2017 lengo likiwa ni kukuza shughuli za kitafiti na kibunifu na kuhaulisha teknolojia, kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

# Mbaroni madai kumiliki karakana ya silaha

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kumiliki karakana ya kutengeneza silaha za kienyeji aina ya gobole bila kibali na kuziuza kwa wahalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema kufuatia msako uliofanyika katika Kijiji cha Chilendu, Kata na Tarafa ya Kibakwe Wilaya ya Mpwapwa walikamatwa watuhumiwa hao, ambao majina hayakutajwa, wakimiliki karakana ya kutengenezea silaha za kienyeji aina ya gobole bila kibali.

Alisema watuhumiwa walikamatwa wakiwa na gobole tano zilizo tayari, baruti gramu 408, goroli vipande vya chuma 40, fremu za silaha mbili na vifaa mbalimbali vya uchongaji wa silaha hizo.

Aidha, alisema katika tukio lingine, mali mbalimbali za wizi zilikamatwa na kuokolewa mikononi mwa wahalifu katika msako na operesheni ni pikipiki za wizi tisa, pikipiki zinazotumika katika uhalifu tano, bangi kilo 5.2, gongo lita 24, mtambo wa gongo moja, televisheni mbili na kompyuta mpakato ( Laptop) mbili.

Aliwataka wananchi walioibiwa wafike katika vituo vya Polisi ili kutambua mali zao zilizoibwa.

Kamanda Lyanga pia akizungumzia matukio mawili ya mauaji kwa nyakati tofauti.

Alisema katika tukio lililotokea Juni 15, mwaka huu kondakta wa daladala Juma Hamisi (25), aliuawa kwa kupigwa na jiwe kichwani na mtuhumiwa ambaye alikuwa ni dereva wa daladala.

Alisema tukio hilo lilitokea Mtaa wa Mjimpya Jiji la Dodoma, ambapo marehemu aliuawa wakati kwa kupigwa na jiwe kichwani wakiwa wanagombea abiria.

Alisema ulifanyika msako na mtuhumiwa alikamatwa Juni 19, mwaka huu akiwa mafichoni katika Kijiji cha Galapo Wilaya ya Bahati mkoani Manyara, na kwamba ambapo tayari mtuhumiwa amefikishwa mahakamani kwa kosa la mauaji. Alisema katika tukio la pili la mauaji Hisaniel Mbwambo (40), Mkazi wa Chang'ombe aliuawa kisha muuaji kutorokea mafichoni.

Alisema msako mkali ulifanyika na kumkamata mtuhumiwa Juni 29, mwaka huu majira ya usiku akiwa mafichoni kambi ya wavuvi katika bwawa la Nyumba ya Mungu Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Vilevile, alisema taratibu za kiupelelezi zikikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Katika tukio lingine, alisema Juni 29, mwaka huu Mtaa wa Nzuguni C, mwanamke mwenye umri wa miaka 28, aligundulika kuwa ameuawa na mwili kutupwa katika kichaka.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha alibakwa kabla ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali shingoni upande wa kushoto na msako kwa waliofanya tukio hilo unaendelea.




Katibu Mtendaji wa UNESCO, Prof. Hamisi Malebu, akizungumza na wananchi wa Kata ya Buigiri wilayani Chamwino (hawapo pichani), kwenye semina iliyowakutanisha viongozi mbalimbali wa serikali, dini juzi. Wapili kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Wakulima mil. 1.9 wasajiliwa kimtandao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesajili wakulima 1.979,662 na maofisa ugani 6,840 kupitia mfumo wa kielektroniki wa M -Kilimo ili kuwatambua na kuongeza wigo wa kuwahudumia wakulima na wadau wengine katika sekta ya kilimo.

Aidha, mikoa mitano ya Morogoro, Njombe, Mara, Tabora na Kilimanjaro imeongoza kwa kusajili wakulima wengi kwenye Mfumo wa M-Kilimo ulioanza kufanya kazi ya kuwajua wakulima wake nchini.

Hayo yalibainishwa jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Mfumo wa M-Kilimo namna unavyofanya kazi katika sekta ya Kilimo.

Alisema wakulima ambao wamesajiliwa katika mfumo huo wameweza kuwasiliana ikiwamo kuuliza maswali na kupata majibu ya changamoto za uzalishaji na masoko ambazo zinawakabili.

Aidha, alisema mfumo huo umewezesha kusajili maofisa kilimo katika ngazi zote kuanzia sekretarieti za mikoa, halmashauri, kata na vijiji.

"Mfumo huu utasaidia kupima utendaji kazi wa maofisa ugani katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji kuwa na takwimu zinazoonyesha kwenye mfumo huu kwa kila ushauri watakaotoa kwa wakulima," alisema Bashe.

Alifafanua zaidi ya kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wakulima wote wanasajiliwa kwenye mfumo huo, huku akisisitiza wakuu wote wa mikoa kuhakikisha wanazisimamia halmashauri kuwezesha wakulima kusajiliwa.

Bashe alitaja mikoa inayoongoza kwa kusajili wakulima ni Morogoro, Njombe, Mara, Tabora na Kilimanjaro, huku mikoa ambayo iko chini

katika kusajili wakulia ni Pwani, Iringa, Mtwara, Tanga na Arusha.

Alisema pia faida za Mfumo wa M-Kilimo ni kurahisisha mawasiliano kati ya mkulima, mfugaji, mvuvi na ofisa ugani, kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi kuyafikia masoko ya mazao kwa urahisi na kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi na wadau wengine wa sekta ya kilimo katika mnyororo wa thamani.

Hata hivyo, alisema mfumo pamoja na kupata mafanikio makubwa ya utendaji kazi, lakini bado kuna changamoto kama vile ya shida ya mtandao katika baadhi ya maeneo nchini, ambapo alisema wizara inaendelea kufanya jitihada ya kuwasiliana na muhusika ili kushughulikia.

Alisema wizara itaendelea kuwajengea uwezo maofisa ugani katika kutumia mfumo ikiwa pamoja na kuwapatia simu za Smartphone kama ambavyo wizara imeweka vipaumbele vyake katika bajeti ya 2021/2022.

Mratibu wa masuala ya M-Kilimo, Rajabu Mkarange, kutoka idara ya mafunzo, huduma za ugani, alisema mfumo huo ni wa kidigatali ambao unamsaidia mkulima kuwasiliana na ofisa ugani ili kutatua kero zinazomkabili.

Mkarange alisema mfumo huo utawasaidia wakulima na maofisa ugani kuweza kuwasiliana kirahisi kutatua changamoto mbalimbali ambazo wanakutana nazo.



# Vijiji 82 wilayani Mbarali vyaunganishiwa umeme

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

JUMLA ya vijiji 82 kati ya 102 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali vimeunganishiwa umeme ambapo vijiji 20 vilivyobaki mchakato wa kuviunganisha umeanza.

Kwa mujibu wa Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Nicodemusi Kapange, wanaendelea na jitihada za kuhakikisha vijiji vyote 20 vilivyosalia vinapata umeme, huku vitongoji navyo vikiunganishwa.

Kapange alisema wanaendelea kuhamasisha wananchi kuepuka vishoka, ambao hupita majumbani wakidai ni maofisa TANESCO na kuwaunganishia umeme kwa gharama kubwa.

Alisema bei elekezi ya kuunganisha umeme ni shilingi 27,000, na kwamba tangu mtu analipia inachukua siku 30 mteja kuunganishiwa.

"Tunaendelea na mchakamchaka wa kuwaunganishia wateja umeme, naamini vijiji vyote 102 vitaunganishwa na huduma kikubwa wananchi kuepuka vishoka ambao hujifanya watumishi wa TANESCO huwaunganishia watu kinyemela, tunaendelea na misako wanaobainika tunawashughulikia kwa mujibu wa sheria," alisema Kapange.

Aliwashauri wananchi fedha za malipo ya kuunganishiwa umeme zilipwe katika ofisi za TANESCO badala ya kumkabidhi mtumishi mtaani, kwani zinaweza zisifikishwe kwenye eneo husika.

Aliongeza hadi sasa wamebadili nguzo 232 zenye urefu wa mita 12 na wamekata miti iliyo kwenye njia kuu ya umeme umbali wa kilometa 234, lengo likiwa kuhakikisha tatizo la kukatika umeme Mbarali linakuwa historia.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimtaka Meneja wa TANESCO kuendelea kuboresha miundombinu ya umeme ili tatizo la kukatika kwa umeme liwe la kihistoria.


Aidha, alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kuwatumia vishoka ili kuunganishiwa umeme badala yake wafike ofisi za shirika hilo ili kupewa wataalamu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na timu yake, amekuwa akitoa ushirikiano mkubwa, na tunakoelekea tatizo la umeme litakuwa historia.

"Nitoe wito kwa wananchi kubadilika, hakuna malipo ya serikali yanayofanyika mkononi, malipo yote yanafanyika kwa kutumia control namba ambayo unapewa na TANESCO na kwa wale wanaofanya ujanja ujanja nawaomba wananchi wawe wanatoa taarifa mapema ili tuwashughulikie."

Katika hatua nyingine, Mfune alisema Serikali imetoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya.

Alisema ujenzi wa wodi hizo utasaidia kukabiliana na uhaba wa vyumba vya kulazwa wagonjwa katika hospitali hiyo na kuwahakikishia wananchi kuwa wataendelea kupata huduma bora za matibabu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, aliwasisitiza wananchi kuchukua hatua dhidi ya ugonjwa wa corona na kuwahamasisha kufuata taratibu zote za afya zilizotelewa na viongozi wakuu wa nchi pamoja na Wizara ya Afya zikiwamo kuvaa barakoa sehemu zenye mikusanyiko, kuepuka misongamano isiyo ya lazima na kufanya mazoezi ili miili izidi kuwa imara.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Loema Peter (wapili kushoto), akimkabidhi hundi ya shilingi milioni 210 mmoja wa wanufaika wa mikopo inayotolewa na halmashauri hiyo juzi. Watatu kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mpokigwa Mwankuga. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Rungwe yakopesha makundi mil. 200/-

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

ZAIDI ya shilingi milioni 200 zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa vikundi 31 ambavyo ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Rungwe, Omary Mungi, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya shilingi milioni 848 zilitolewa kwa vikundi 123 na kuvinufaisha vikundi vya wanawake 79, vijana 40 na watu wenye ulemavu vikundi 4.

Akizungumza jana wakati wa kutoa mkopo wa shilingi milioni 200 kwa vikundi 31, Mungi alisema marejesho ya fedha zilizotolewa awali yalikuwa mazuri na kwamba wana imani na wanufaika wa sasa watarejesha kwa wakati.

Aliwaomba wanufaika kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kufanya biashara walizozibainisha wakati wa kuomba mkopo badala ya kuzitumia kwenye mambo mengine ikiwamo ya anasa.

"Kuna watu hapa wameshawaambia nyumbani kuwa tumepata fedha hivyo wawe tayari kula nyama na kuvaa nguo nzuri, niwaonye! Fedha hizi zitumike kwa malengo yaliyoombewa, muwe wabunifu kwa kuanzisha vitega uchumi vitakavyosaidia mle nyama siku zote maisha yenu yote na si vinginevyo," alisema Mungi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliomba wanufaika kuwa wabunifu katika bidhaa wanazozitengeneza ili zikidhi mahitaji ya soko la ushindani ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter, alisema halmashauri imeendelea kutoa mikopo hiyo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM, na kuwomba wananchi kulipa kodi ili serikali ipate fedha za kutoa mikopo.

# TMDA kudhibiti uingizaji wa dawa, vifaa tiba hafifu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imejipanga kudhibiti uingizwaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kuhakikisha wanaongeza ulinzi na ukaguzi maeneo ya mipakani.

Maeneo hayo ni mpaka wa Tunduma uliopo mkoani Songwe na Kasumulu uliopo mkoani Mbeya.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mratibu wa Ofisi za Kanda za TMDA, Dk. Henry Irunde, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wakaguzi wa dawa ngazi ya halmashauri ambayo yaliwahusisha wafamasia na madaktari wa binadamu na mifugo mkoani Songwe.

Alisema mikoa ya Songwe na Mbeya inahitaji kazi kubwa ya kufanya katika udhibiti na uingizwaji wa dawa kwa madai kuwa maeneo ya mipaka watu wasiokuwa waaminifu huitumia kuingiza bidhaa zilizokwisha muda wake au zisizokuwa na ubora.

Alisema TMDA kwa kushirikiana na wakaguzi wa halmashauri ambapo walipewa vyeti vya utambulisho ili kutekeleza majukumu ya ukaguzi, watafanya kazi ya kukagua maduka, hospitali, maabara na mipaka ili kuangalia bidhaa hizo kama zinafaa kwa matumizi ya binadamu.

Irunde alisema moja ya maeneo yanayochangia uingizwaji wa dawa na vifaa tiba bandia ni kutokuwapo kwa ushirikiano katika kudhibiti uzalishaji na uingizwaji wa bidhaa hizo, ambazo huingizwa kwa njia ya panya.

"Ninawaomba watumishi mliopatiwa mafunzo na TMDA namna ya kufanya ukaguzi, kuzingatia maadili ya kazi katika kukabiliana na vifaa tiba bandia na utoaji wa taarifa kuhusiana na bidhaa hizo hatua hiyo, itasaidia kudhibiti uzalishaji na uingizwaji wa bidhaa zilizopigwa marufuku," alisema Dk. Irunde.

Kaimu Meneja wa TMDA, mikoa ya nyanda za juu kusini, Anitha Mshighati, alisema moja ya mikakati waliyoiweka ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili kudhibiti uingizwaji wa dawa bandia.

Alisema kwa kuwa wakaguzi hao ni watendaji wa halmashauri, anaamini baada ya mafunzo hao watakwenda kukabiliana na kudhibiti mianya yote iliyokuwa inatumika kuingiza bidhaa zilizopigwa marufuku.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Nyembea Hamad, alisema uwekezaji wa viwanda vya vifaa tiba nchini utasaidia kupunguza tatizo la dawa na vitendanishi bandia.

Aliwaomba wawekezaji kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika dawa ili kukabiliana na tatizo ya bidhaa zilizopigwa marufuku ili kuokoa maisha ya wananchi.





## SMZ yaingia mfumo malipo kwa mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, amesema serikali imeingia rasmi katika matumizi ya mifumo ya kidigitali ya malipo, huku akiwataka wananchi kuwa tayari kuendana na mabadiliko hayo.

Aliyasema hayo jana Bandarini Wete Pemba wakati akizindua mfumo mpya wa malipo kwa wakulima wa karafuu kupitia huduma ya Ezypesa, ambapo wakulima watalipwa malipo yao kwa njia ya simu tofauti na ilivyo sasa.

Alisema serikali imeamua kutumia mifumo ya kidigitali katika malipo na makusanyo yate ya fedha, kama ilivyotolewa na Waziri wa Fedha barazani mwaka huu.

Waziri Omar alisema hakuna fedha yoyote ya mkulima itakayotolewa mkononi, bali wakulima watalipwa fedha zao kutumia Mfumo wa Ezypesa, huku akiyataka mashirika hayo kujizatiti katika mifumo yao ya malipo isije ikawa ni changamoto kwa wakulima wakati wa kuhitaji fedha zao.

"Suala la mfumo wa malipo hapa lazima wananchi na wakulima mfahamu, serikali imeamua kwenda na mfumo wakidigitali kuanzia mwaka huu, hakuna fedha itakayotoka mkononi fedha zitatumia mifumo ya kisasa," alisema.

"Tunajua mfumo huo ndio umeanza na mgeni kwetu sisi, unaweza kuleta changamoto, changamoto zitakazojitokeza zitatatuliwa kwa wakati," alisema.

Aliitaka Zantel na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kujipanga kikamilifu kuhakikisha mifumo ya malipo inakuwa sawa na wananchi hawapati matatizo wanapopokea malipo yao.

Ofisa Mkuu wa Fedha Zantel, Azizi Said Ali, alisema kampuni ya Zantel iko mstari wa mbele katika kuhakikisha wateja wake wanapata huduma bora za kidigitali na bei nafuu, ili kurahisisha maisha kwenye ulimwengu wa sasa wa kidigitali.

# Changamoto Mkoa wa Kusini zamgusa Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekamilisha ziara yake Mkoa wa Kusini Unguja na kusema kuwa amekuta changamoto nyingi zinazowakabili wananchi katika mkoa huo. Dk. Mwinyi alisema hatovumilia kuziona changamoto hizo za kiutendaji na atachukua hatua kwa wasiotaka kuwajibika.

Aliyasema hayo juzi kwa nyakati tofauti wakati akisikiliza changamoto za wananchi wa Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja akiwa katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

"Utendaji haupo kwa sababu gani, hii ni ziara yangu ya kwanza pengine hamjanitambua natoa ujumbe kwa huko ninakokwenda yakitokea haya yaliotokea hapa nitawafukuza watu hadharani sitawaacha hata kidogo," alisema.

Aliwataka watendaji kufanya kazi walizopewa na kama hawawezi kufanya kazi wapo huru kujiuzulu ili kazi walizopewa wapewe watu wingine.

Aidha, alisema serikali inatambua kuwapo kwa mgogoro wa ardhi unaowahusisha wananchi wa Shehia ya Ubago dhidi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kambi ya Ubago. Akizungumza na wananchi wa shehiya za Ubago, Dunga na Binguni, baada ya kukagua ujenzi wa Hospitali ya Rufani Binguni, Mkoa wa Kusini Unguja, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake, alisema serikali imeunda tume maalum kwa ajili ya kufanya uchunguzi kuhusiana na mgogoro huo.

Alisema uchunguzi huo utakapokamilika, taarifa zake zitawasilishwa serikalini kwa hatua za kuupatia ufumbuzi wa kudumu mgogoro huo.

Alisema kazi za ulinzi wa nchi ni muhimu katika mustakabali wa usalama wa taifa, hivyo akawataka wananchi kuelewa kuwa hata maeneo yanayoonekana kuwa wazi, kuna shughuli muhimu za kiulinzi, hivyo akabainisha umuhimu wa wananchi kuishi mbali na maeneo ya jeshi.

Aliwataka wananchi hao kuwa na subira, na kuahidi serikali kufanya maamuzi pale taarifa zitakapowasilishwa serikalini, huku akiwaomba wananchi hao kuondokana na mivutano.

Aidha, alisema serikali itafuatilia kubaini changamoto ya wananchi wa Dunga Kiembeni Bondeni, wanaodai kutoa kiasi cha shilini milioni 12 kwa ajili kufungiwa umeme na baada ya kukamilika mchakato wa kuwekewa miundombinu na kuanza kupata huduma hiyo, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) limefika na kuondoa miundombinu hiyo.

Akizungumza na wakulima wa Bonde la Mpunga Cheju linaloendesha mradi mkubwa wa uwekaji wa miundombinu ya kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji, alisema pamoja na mradi huo kuchelewa kuanza, kuna matumaini makubwa ya mradi huo kukamilika Aprili 2022 na kuleta tija kubwa kwa wakulima.

Aliwataka wakulima wa bonde hilo kuondokana na utegemezi wa kuitegemea serikali kwa kila kitu, ikiwamo kupatiwa pembejeo, na kubainisha kazi kubwa iliyofanywa na serikali ya kuwawezesha wakulima hao.

Rais Dk. Mwinyi aliuagiza uongozi wa Wizara ya Kilimo kufanya uchunguzi ili kubaini viongozi waliohusika kuhodhi maeneo makubwa ya kilimo katika bonde hilo na kutaka kufikishiwa taarifa hizo, hatua iliokuja baada ya wananchi kulalamika kuwapo viongozi waliohodhi maeneo makubwa kwa lengo la kujinufaisha.

Aidha, aliutaka uongozi wa Wizara ya Kilimo, kukutana na wakulima wa bonde hilo ili kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili, huku akiahidi serikali kusimamia mradi huo ili kukamilika kwa wakati.

Dk. Mwinyi, alisema serikali itaendelea kutimiza wajibu wake wa kushughulikia miradi mikubwa ya kijamii, ikiwamo kuimarisha huduma za majisafi na salama, elimu pamoja na upatikanaji wa huduma za afya.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano, Uchukuzi na Usafirishaji, Rahma Kassim Ali, alisema katika mwaka 2021/2022 serikali imepanga kuzifanyia matengenezo barabara 220 za ndani kwa kiwango cha lami ikiwamo zilizotemebelewa na Rais Dk. Mwinyi na kuondokana na utaratibu wa ujenzi wa kifusi usio tija.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Soud Nahoda, alisema kukamilika uwekaji wa miundombinu ya kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji katika Bonde la Cheju, kutaongeza kiwango cha uzalishaji mpunga hapa nchini kutoka asilimia 30 na hadi 60.

Dk. Mwinyi anaendelea na ziara yake katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa siku mbili kisha kutembelea mikoa mingine ya Unguja na Pemba.



Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akimtambulisha kwa wananchi mgombea ubunge wa Jimbo la Konde kupitia chama hicho, Muhamed Said Issa, katika mkutano wa hadhara wa ufunguzi wa kampeni uliofanyika katika Viwanja vya Konde Polisi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaosaka uongozi CCM 2022 kufanyiwa tathmini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka wanachama wa chama hicho kuacha kutengeneza safu za uongozi, chama kitahakikisha kinapata viongozi wanaowajibika ikiwamo kushiriki kwenye vikao.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wanachama katika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui ikiwa ni ziara yake ya kwanza ya kujitambulisha, baada ya kushika nafasi hiyo.

Alisema CCM inakabiliwa na uchaguzi wa viongozi mwakani, hivyo chama hicho, kinatarajia kuandaa waraka maalumu wa kuwatathmini viongozi wanaoomba uongozi kuangalia ushiriki wao katika vikao vya chama kwenye ngazi ya chini.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupata viongozi ambao wana mwonekano mzuri katika kuendesha chama chao na wasipofanya hivyo watapata viongozi sio bora na kuanza kulaumiana.

Aidha, aliwataka wanachama hao kujitokeza kwa wingi kutimiza haki yao ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa.

Alisema kazi ya CCM ni kutengeneza uongozi ambao walishaikamilisha tokea mwaka 2020, ambapo kwa sasa wana wajibu mkubwa wa miaka mitano wa kufanya kazi ya msingi ya kusimamia ilani ya uchaguzi.

"Tukiangaliana kwa aibu, tusipofanya ufuatiliaji wa karibu wa miradi ya maendeleo sisi ndio tutaulizwa mwisho na sisi ndio tunaomiliki duka... tukiwaacha wauzaji wauze kiholela mwishoni tutaopata hasara ni sisi, na hasara hiyo sisi tuliopewa jukumu hatuko tayari kuona likitukabilimwishoni," alisema.

Naye Naibu wa CCM Tanzania Bara, Christina Mdene, alisema sifa ya kiongozi ni kuweka milango wazi ya kusikiliza kero za wananchi kama ambavyo ilani ya chama chao ibara ya 251(i) inavyoelekeza.

Aliwataka viongozi kutenga muda japo wa siku moja kushuka chini na kwenda kwa wananchi kusikiliza kero zao ambazo zinawakabili ili kupatiwa ufumbuzi.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Mabodi, aliwahimiza viongozi wasibweteke, badala yake washuke chini kuwafikia wananchi ambao waliwachagua.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ISMAIL YUSUF ISMAIL** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 177438** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Arusha tarehe mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/334527/2021.**

116346402

## VYETI VIMEPOTEA



**YOHANA MABULA LUCAS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0539/0221** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MAGU SEKONDARI mwaka 2013. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0968/0549** kilicholewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MATAKA SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayevio-na atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NY/RB/794499/2020.**

1163345102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Pendo Mabula Daudi** mkazi wa Kizumbi Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **V-ROX** jina la Kadi Kahama Import yenye namba za usajili **MC 237 BLQ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Pendo Mabula Daudi kwa simu namba **0769847910.**
**Rbnamba Shy/RB/ 2021,**
**Control namba 9910825329907.**

116346102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NGAO KAHEMA MBWANJI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NISSAN ATLAS YENYE NAMBA ZA **USAJILI T.969 AGF.** CHASSIS NAMBA **MH40066267.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBA/RB/333875/2021**

116344902

## ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA **TAREHE 04/08/2021** SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA **CROWN MAJESTA T 997 DCM** MALI YA SELEMAN MSIGALA, MAENEO YA NYERERE SQUARE (MAJI YA CHAI), BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841.**

116344802

## KUPOTEA KWA VYETI



**NOBERT ARON RUTAMIKA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifutavyo,cha kidato cha nne chenye index namba S **0967-0237** kiichotolewana baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MLOLE mwaka 2011,na cheti cha kidato cha sita index namba **S 0132-0718** kilichotolewa na shule ya secondary MILAMBO mwaka 2014,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **KGT/CPS/B1/VOL11/122/2021**

116344202

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi NA. 63/2021**

**Ombi la MWAJABU HAMISI ALLY kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu BAKARI MOHAMEDI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 12/07/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 25/06/2021

Tarehe ...25/06...20...21......
........................
**Sahihi ya Hakimu**

116344702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDUGU CHARLES FAURSRINE RWAGASINGIRE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T897AZH** aina ya MITSUBISHI CANTER Rangi Mult COlour yenye Chasis No. **FE315BD464285.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/DOD/RB/330898/2021**

116344602

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHILIPO DALIKACHUMA** LUHWAGO ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 377 AHN.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MOR/GAI/RB/280625/2021.**

116344302

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Idriss Déby azuru Ufaransa

**Paris,** UFARANSA

RAIS wa Chad Mahamat Idriss Déby amezuru Ufaransa anakokutana na mwenyeji wake Emmanuel Macron, kujadiliana masuala mbalimbali yenye maslahi kati ya nchi hizo mbili.

Taarifa kutoka Ikulu ya Élysée, imesema viongozi hao wawili watazungumzia hali ya siasa nchini Chad, kuelekea uchaguzi mkuu ujao.

Rais Emmanuel Macron na Mahamat Idriss Déby Itno watajadiliana pia hali ya usalama katika ukanda wa G5 Sahel. Mataifa ya G5 Sahel ni pamoja na Burkina Faso, Chad, Mali, Mauritania na Niger.

Ufaransa imetuma wanajeshi wake katika eneo hilo kukabiliana na makundi ya kijihadi, wakati huu Rais Macron akitangaza kupunguza kikosi kinachoshiriki kwenye operesheni inayoitwa, Barkhane.

Wiki kadhaa zilizopita, Mahamat alisema Chad itaendelea kuonyesha uongozi katika mapambano dhidi ya makundi ya kijihadi na imetuma wanajeshi wake nchini Mali inakoshirikiana na vikosi vya Ufaransa.

Baba yake Itno, Idriss Deby, alifariki dunia Aprili mwaka huu, akiwa kwenye uwanja wa mapambano akiongoza jeshi la nchi yake dhidi ya wanajihadi Kaskazini mwa nchi hiyo.

**RFI**

# TB Joshua kuzikwa kwa faragha

**Lagos,** NIGERIA

TARATIBU za mazishi ya aliyekuwa muhubiri mashuhuri wa Nigeria na Mwasisi wa Kanisa la Synagogue Church of All Nations (SCOAN), TB Joshua, aliyefariki mwezi uliopita, zimeanza kwa tukio la kuwasha mishumaa jana.

Mazishi yake yanatarajiwa kuwa ya faragha yatakayofanyika Ijumaa Julai 11, mwaka huu.

TB Joshua alifariki Juni 5, akiwa na umri wa miaka 57, siku chache kabla ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa.

Mchakato wa kuwasha mishumaa utakuwa ni sherehe ya kibinafsi, limesema kanisa hilo.

Tukio hilo lilitarajiwa kuanza saa 12:30 jioni jana saa za Nigeria.

Kanisa hilo limewataka watu kubeba mishumaa kama ishara ya kuungana katika mpango wa kumheshimu mtumishi wa Mungu, TB Joshua.

**BBC**



# Zuma afananisha hukumu yake na kifo

**Kwa-Zulu Natal,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma (79), aliyetakiwa kujisalimisha gerezani ili kukitumikia kifungo cha miezi 15 kwa kuupuza amri ya Mahakama, amesema hatotii hukumu hiyo.

Amesema kwa umri alionao hukumu hiyo ni sawa na kumpa hukumu ya kifo.

Wiki iliyopita, Mahakama ya Katiba ilimpa adhabu hiyo Rais Zuma, kwa kutoheshimu agizo la mahakama kutoa ushahidi kwa tume, iliyokuwa inachunguza madai ya ufisadi alipokuwa rais kati ya mwaka 2009 hadi 2018.

Akizungumza katika mkoa wa Kwa-Zulu Natal alikozaliwa, Zuma amewafananisha majaji waliotoa hukumu dhidi yake, kama viongozi waliongoza taifa hilo wakati wa kipindi cha mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi.

"Hakuna haja ya mimi kwenda jela, kunifunga katika kipindi hiki, kwa umri wangu ni sawa na kunipa hukumu la kifo," alisema Zuma.

Zuma, alipaswa kujisalimisha gerezani Jumapili, lakini mahakama imekubali kusikiliza rufani ya kupinga kifungo hicho cha miezi 15.

Wafuasi wake wameapa kutokubali kufungwa kwa kiongozi huyo wa zamani huku wakitengeneza ngao nje ya nyumba yake ili kuzuia kiongozi huyo asikamatwe.

Jumanne iliyopita Mahakama ya Kikatiba ilimkuta Zuma na hatia ya kudharau agizo la mahakama la kuhudhuria kwenye kesi yake ya madai ya ufisadi na kumpa adhabu ya kifungo cha miezi 15 jela.

Mahakama ya Katiba ilisema kwamba ilipokea ombi la kukata rufani la Zuma Ijumaa na italifanyia maamuzi ya ombi hilo mnamo Julai 12.

Taasisi ya Jacob Zuma, mfuko wa misaada wa rais wa zamani, ilisema rufani dhidi ya amri ya kukamatwa itasikilizwa na Mahakama Kuu ya jimbo la KwaZulu-Natal leo.

Jacob Zuma 79 aliondolewa mamlakani mnamo 2018, baada ya miaka tisa madarakani, akikabiliwa na shutuma za ufisadi.

Wafanyabiashara walishutumiwa kwa kula njama na wanasiasa kushawishi mchakato wa kufanya uamuzi.

Zuma alikana shutuma zilizomkabili katika kesi yake ya ufisadi iliyohusisha makubaliano ya silaha ya thamani ya dola bilioni 5 kutoka miaka ya 1990.

Umati wa wafuasi umekusanyika nje ya nyumba yake kuhakikisha kuwa hapelekwi gerezani.

Chama tawala cha Afrika Kusini cha ANC, ambacho Zuma alikuwa akiongoza, kimetaka utulivu. Lakini akiogopa mgongano katika mkutano wa kamati yake kuu ya kitaifa ambao umeahirishwa wikiendi hii.

**BBC/RFI**




Vyombo vya habari vikiwa vimekusanyika jana, nje ya Hospitali ya Kikatoliki ya Gemelli Polyclinic. Papa Francis anapatiwa huduma katika hospitali hiyo baada ya kulazwa juzi na kufanyiwa upasuaji wa utumbo mkubwa. **PICHA: AP**

# Papa aendelea vizuri baada ya upasuaji utumbo saa 3

**Roma,** ITALIA

VATICAN imesema kuwa Papa Francis ana hali nzuri na anapumua mwenyewe bila usaidizi, baada ya upasuaji wa kuondoa sehemu ya utumbo mkubwa uliochukua saa tatu kutokana na ugonjwa ujulikanao 'colon diverticulum stenosis'

Papa Francis, 84, katika upasuaji ilibidi apigwe 'nusu kaputi', msemaji wa Vatican Matteo Bruni, amesema.

Ni mara ya kwanza Papa Francis kulazwa hospitalini tangu kuchaguliwa kwake kuwa kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, mwaka 2013.

Mapema Jumapili, Papa ambaye ni raia wa Argentina alihutubia maelfu ya wageni katika uwanja wa St Peter's, taarifa iliyotolewa awali na Vatican ilisema, Papa Francis alikuwa anatibiwa katika hospitali ya chuo kikuu cha Gemelli kwa tatizo la utumbo mpana.

Ugonjwa huo ni hali inayojumuisha vifuko katika ukuta wa utumbo mpana na kusababisha kupungua na dalili zake ni pamoja na utumbo kuvimba, kuwa na maumivu na mabadiliko ya tabia za utumbo.

Vatican haikutoa maelezo zaidi kuhusu upasuaji huo au kipindi ambacho Papa anatarajiwa kuwa hospitalini.

Wakati wa ibada ya Jumapili katika Kanisa la Mtakatifu Petro, Papa alitangaza kuwa ataenda Slovakia, Septemba mwaka huu, baada ya kufanya ibada Budapest, mji mkuu wa Hungary.

Papa Francis mwaka 1936 akiwa Buenos Aires na alifanyiwa upasuaji na kuondoa sehemu ya pafu lake la upande wa kulia akiwa na umri wa miaka 21.

Pia aliwahi kupata tatizo la nyonga na siatika (ugonjwa wa mshipa wa nyuma ya paja), unaosababisha maumivu kuanzia sehemu ya chini ya mgongo hadi miguuni.

Mwaka 2014, alilazimika kuahirisha shughuli zake kadhaa kwa sababu ya maradhi ya tumbo.

Awali Kardinali Enrico Feroci kutoka Italia aliwaambia waandishi wa habari kuwa Papa yupo vizuri: "Maombi yetu ni makubwa kwake," akiwa Roma.

Taarifa kutoka Vatican, iliripotiwa kuwa Papa alipelekwa katika Hospitali ya Gemelli hapo awali.

Baada ya habari kwamba Papa alikuwa amelazwa hospitalini, ujumbe wa "upone haraka" umekuwa ukitolewa na viongozi mbalimbali. Taarifa zinasema atakaa hospitalini kwa siku tano.

Rais wa Italia Sergio Mattarella, Rais wa Malta George Vella na Rais wa Bunge la Ulaya David Sassoli ni kati ya viongozi waliotuma ujumbe wa ugua pole kwa Papa.

**AP/TRT**



# POGBA BADO SANA JUVE

**TURIN, Italia**

MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Juventus, Fabio Paratici, amesema mabingwa hao wa Serie A kamwe hawajawahi kukaribia kumsajili tena nyota wa Manchester United, Paul Pogba.

Pogba anaingia kwenye mwaka wake wa mwisho pale United na nyota huyo wa Ufaransa majaliwa yake bado yamebakia kuwa na sintofahamu, huku akihusishwa na Juventus, Real Madrid na Paris Saint-Germain.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye aliondoka United kwenda Juve mwaka 2012 kabla ya kurudi Old Trafford mwaka 2016, kwa muda mrefu amekuwa akihuishwa na 'Bianconeri' hao, lakini Paratici ametupilia mbali uvumi huo.

"Paul Pogba kurudi Juventus? Nafikiri ni ngumu sana," alisema Paratici, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Soka pale Tottenham, akiambia Sky Sport.

"Kamwe hakujakuwa na muda ambao tulikaribia kumsajili na kumrudisha tena Juventus."

Pogba na Ufaransa walitolewa kwenye michuano ya Euro 2020 hatua ya 16-bora na Uswisi kwa mikwaju ya penalti baada ya muda wa kawaida na ule wa nyongeza kumalizika kwa sare.

## SPURS WAPAMBANA KUMBAKISHA KANE



**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur wana kocha mpya na mkurugenzi mpya wa soka, lakini wamesisitiza kuwa wanaangalia uwezekano wa kuhakikisha wanambakisha straika wao, Harry Kane.

Uvumi umekuwa ukisambaa kuhusu majaliwa ya Kane ambaye amebainisha wazi kuwa anataka kuondoka, huku Spurs ikiripotiwa kukataa ofa ya pauni milioni 100 kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City mwezi uliopita.

Pia klabu za Chelsea, Manchester United, Real Madrid, Barcelona na Paris Saint-Germain zimekuwa zikihusishwa na nia ya kuwania saini yake.

Lakini Mkurugenzi wa soka wa zamani wa Juventus, Fabio Paratici ambaye kwa sasa yupo kwenye nafasi kama hiyo pale Tottenham – amemsifia Kane, akisema Spurs wanataka kumbakisha nahodha huyo wa England wakati Nuno Espirito Santo akichukua mikoba hapo London.

"Kumbakisha ni moja ya malengo yangu, ni malengo ya klabu," alisema Paratici akiiambia Sky Sports.

"Kamwe siwezi kusubiri kumWangalia mubashara, nimekuwa na bahati kwa miaka kadhaa iliyopita kwa sababu nimewashuhudia mastraika wakubwa kama Cristiano Ronaldo, Carlos Tevez, Alvaro Morata, Gonzalo Higuain, na wengine wengi ambao nimewasahau.

"Kwa sasa, yeye ni mmoja wa mastraika bora duniani. Ni mchezaji aliyekamilika, kwa hakika kabisa. Ni mchezaji mwenye nguvu na namba tisa wa uhakika, mwenye njaa ya bao na ufundi mwingi.

"Ni mchezaji wa aina yake, lakini ni mmaliziaji mzuri sana, kwa uhakika naamini yeye ni mmoja wa wachezaji bora watatu duniani."

## HERNANDEZ APASULIWA GOTI

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imethibitisha mlinzi wake, Lucas Hernandez, amefanyiwa upasuaji wa goti.

Mkurugenzi wa michezo Bayern, Hasan Salihamidzic, alisema katika taarifa yake: "Tunamtakia kila la heri Lucas ili apone haraka.

"Madaktari wetu wameridhishwa na maendeleo yake baada ya operesheni yake. Atakuwa tena dimbani ndani ya wiki chache zijazo."

Hernandez amecheza mechi 62 kwa Bayern kwenye mashindano yote tangu ajiunge na miamba hao wa Ujerumani akitokea Atletico Madrid miaka miwili iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alipoteza mchezo mmoja tu kati ya 42 aliyocheza kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Pia hakupoteza mchezo hata mmoja kati ya 25 ya ligi aliyocheza katika msimu wake wa kwanza pale katika dimba la Allianz Arena wakati Bayern wakishinda mataji matatu chini ya Hansi Flick.

Mabingwa hao wa Ujerumani kwa sasa wananolewa na kocha mpya, Julian Nagelsmann, na wataanza kutetea taji lao ugenini dhidi ya Borussia Monchengladbach, Agosti 13, mwaka huu.





# VIEIRA

## KOCHA MPYA CRYSTAL PALACE

**LONDON, England**

KLABU ya Crystal Palace imemtangaza Patrick Vieira kuwa kocha wake mpya kuelekea msimu mpya wa 2021-2022.

Raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 45, amesaini mkataba utakaomweka hapo hadi mwaka 2024, na kocha huyo wa zamani wa Nice amechukua mikoba ya Roy Hodgson pale katika dimba la Selhurst Park.

Kocha wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo alionekana kuwa ndiye mtu sahihi wa kuchukua mikoba hiyo, kabla ya raia huyo wa Ureno kuitosa nafasi hiyo.

Badala yake Nuno akaamua kujiunga na Tottenham, huku Palace pia walikaribia kumchukua kocha wa zamani wa Borussia Dortmund, Lucien Favre, ingawa raia huyo wa Uswisi aliamua kuchomoa nafasi hiyo.

Hata hivyo, Palace sasa wameamua kumchukua gwiji wa zamani wa Arsenal, Vieira, ambaye aliwasaidia 'Washikabunduki' hao kutwaa mataji matatu ya Ligi Kuu England, akisaini mkataba wa miaka mitatu.

"Nina furaha kubwa sana kupata nafasi ya kurudi kwenye Ligi Kuu England, na hii ni klabu kubwa, na tunakwenda kuanza ukurasa mpya pamoja," alisema Vieira akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Msingi wa klabu hii unavutia sana baada ya kuwa kwa miaka mingi kwenye Ligi Kuu, na tuna matumaini tunaweza kufanya mambo makubwa na kupata mafanikio hapa."

Vieira alianza kazi ya ukocha pale Manchester City, ambako pia alimalizia siku zake za kucheza, na baadaye akateuliwa kuwa kocha wa klabu dada ya City, New York City FC ya nchini Marekani mwaka 2015.

Baada ya mafanikio kule kwenye Ligi Kuu Marekani (MLS), Vieira alijiunga na Nice mwaka 2018, akichukua nafasi ya Favre, akiisaidia kumaliza nafasi ya saba na tano katika misimu miwili aliyokaa pale.

Alifukuzwa Desemba 2020, akishinda mechi 35 kati ya 89 aliyoiongoza kwenye mashindano yote na kupoteza 32.

## DESCHAMPS NJIAPANDA MKATABA MPYA UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**



DIDIER Deschamps atafanya mazungumzo na Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), Noel Le Graet wiki chache zijazo baada ya kikosi hicho kuondolewa kwenye michuano ya Euro 2020.

Kabla ya kuanza kwa michuano hiyo, Ufaransa ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo na iliongoza kundi lake lililokuwa na timu za Ureno, Ujerumani na Hungary, na ikatolewa hatua ya 16-bora kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na Uswisi.

Hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza tangu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2010 kwa 'Les Blues' hao kushindwa kufuzu robo fainali kwenye mashindano makubwa.

Kuondolewa mapema kwa Ufaransa kumezua maswali mengi kuhusu majaliwa ya Deschamps, huku Zinedine Zidane akitajwa kuhusishwa na kazi hiyo tangu alipoondoka Real Madrid, Mei mwaka huu.

Mkataba wa sasa wa Deschamps unamalizika baada ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar tangu alipochukua mikoba hiyo mwaka 2012, akibeba Kombe la Dunia mwaka 2018 na kutinga fainali ya Euro 2016.

La Great alinukuliwa wiki iliyopita akisema kwamba, kocha huyo mwenye umri wa miaka 52, nafasi yake haipo shakani, lakini rais huyo wa FFF anapanga kukutana na Deschamps kwa siku chache zinazokuja.

"Tutakutana wiki ijayo. Mara zote naacha siku 10 zipite," La Graet aliiambia Telefoot.

"Tutakutana ofisini kule Guingamp na tutakuwa na siku nzima pamoja. Kila mmoja anatakiwa kufikiri kuhusu nini kipo sawa na kipi hakipo sawa."

Alipoulizwa kuhusu kauli yake ya hivi karibuni juu ya majaliwa ya kazi ya Deschamps, La Graet alisema: "Sikusema hivyo. Nilisema tutakuwa na majadiliano. Tutazungumza kuhusu nini kilichokwenda vibaya."

## LIVERPOOL YAONGOZA KUMWANIA MBAPPE



**LIVERPOO, England**

LIVERPOOL inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa RMC.

Majaliwa ya Mbappe pale kwenye Jiji la Paris yametawala vichwa vya vyombo vya habari kwa siku za hivi karibuni.

Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa na Real Madrid kwa muda mrefu, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, kuweka wazi kwamba hana mpango wa kuongeza mkataba pale PSG.

Mkataba wa Mbappe pale PSG unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22 na amekuwa akihusishwa sana kujiunga na miamba wa LaLiga, Real Madrid.

PSG bado hawajaweza kumshawishi Mbappe kusaini mkataba mpya na nyota huyo wiki iliyopita alinukuliwa akisema kwamba, hana mpango wa kufanya hivyo, kwani anataka kuondoka na kwenda kutafuta changamoto mpya.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti ya RMC ya jana, Jumatatu, Liverpool ndio wanaongoza katika mbio za kuwania kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa ambaye alikosa penalti dhidi ya Uswisi na timu yake kutolewa kwenye Euro 2020 hatua ya 16.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa, Liverpool wanajiandaa kutuma ofa rasmi kwa PSG kwa ajili ya kumsajili kipindi cha dirisha kubwa la majira ya joto.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KISASI ITALIA VS HISPANIA NUSU FAINALI EURO 2020

**Timu hizo mbili zimekutana mara 34 na Wahispania kushinda 12, sare 13, huku Waitalia...**

**LONDON, England**

NUSU fainali ya kwanza ya Euro 2020 inapigwa leo, Jumanne kati ya Italia na Hispania kwenye dimba la Wembley hapa London.

Miamba hao wawili wa Ulaya wamefuzu hatua hiyo baada ya kupata ushindi kwenye mechi zao za robo fainali dhidi ya Ublegiji na Uswisi.

Hispania katika mechi zao tatu zilizopita wamefunga mabao 11 na kikosi hicho cha kocha Luis Enrique (pichani), kililazimika kusubiri hadi kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti ili kufuzu hatua hiyo dhidi ya Uswisi.

Kwa upande wa Italia, imekuwa timu yenye kiwango cha kuvutia zaidi kwenye Euro 2020 hadi sasa.

Kikosi hicho cha kocha, Roberto Mancini kilikuwa kwenye kiwango bora zaidi dhidi ya Ubelgiji na hivyo kujihakikisha kutinga nusu fainali baada ya ushindi wa mabao 2-1.

Timu hizo mbili kwa ujumla zimekutana katika mechi 34 na Hispania imeshinda 12, huku Italia ikishinda mara tisa na 13 wakitoka sare.

Mara ya mwisho timu hizo kukutana ilikuwa ni mwaka 2017 na Hispania walipata ushindi wa mabao 3-0. Kwa kikosi cha Italia, kitamkosa mlinzi wake wa kushoto, Leonardo Spinazzola, ambaye aliumia kifundo cha mguu kwenye mchezo dhidi ya Ubelgiji, huku Hispania ikiwa haina majeruhi yeyote hadi sasa.

Vikosi vinavyoweza kuanza;

Italia (4-3-3): Gianluigi Donnarumma; Emerson Palmieri, Giorgio Chiellini, Leonardo Bonucci, Giovanni Di Lorenzo; Jorginho, Manuel Locatelli, Nicolo Barella; Federico Chiesa, Lorenzo Insigne, Ciro Immobile.

Hispania (4-3-3): Unai Simon; Jordi Alba, Aymeric Laporte, Eric Garcia, Cesar Azpilicueta; Sergio Busquets, Koke, Pedri; Dani Olmo, Ferran Torres, Alvaro Morata.

## KWA UFUPI

**RONALDO KUONGEZA MKATABA**

WAKALA Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes, anafanyia kazi mpango wa kuongezwa mkataba kwa nyota huyo ili abakie Juventus kwa mwaka mmoja zaidi. **(Sky Sport Italia)**

**PJANIC, UMTITI KUONDOKA BARCA**

BARCELONA wako tayari kukatisha mikataba ya wachezaji wake, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31 na mlinzi wa Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 27, ambao wanaonekana hawako kwenye mipango ya kocha, Ronald Koeman. **(Goal)**

**SPURS WAMWANIA PJANIC**

NYOTA wa Barcelona, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31, anahusishwa na uhamisho wa kuelekea Tottenham Hotspur. **(Express)**

**INSIGNE AGOMBEWA ULAYA**

KLABU za Tottenham na Barcelona wanamwania nahodha wa Napoli, Lorenzo Insigne mwenye umri wa miaka 30, ambaye ameng'ara katika michuano ya Euro 2020. **(Corriere dello Sport)**

**COUTINHO AWEKWA SOKONI**

BARCELONA wako tayari kupokea ada kiduchu kwa ajili ya kiungo wake Mbrazil Philippe Coutinho kuliko ile waliyoilipa Liverpool wakati nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, alipojiunga na wakali hao wa La Liga, kwa sasa thamani yake inaendelea kushuka. **(Sky Sport)**

**RYAN ANUKIA SOCIEDAD**

GOLIKIPA wa Brighton, Mat Ryan mwenye umri wa miaka 29, ambaye aliichezea Arsenal kwa mkopo msimu uliopita anakaribia kutua Real Sociedad. **(Sky Sports)**

**WILLOCK ATAKIWA NEWCASTLE**

MLINZI wa zamani wa Newcastle, Steve Howey, anasema klabu hiyo lazima imsajili kiungo Joe Willock mwenye umri wa miaka 21, msimu huu au wawe katika hatari ya kumkosa kabisa huko mbeleni, kwa sababu ya vita ya bei ya nyota huyo wa Arsenal ni kubwa. **(Chronicle)**

**MENDY AMENDEWA INTER**

MLINZI wa kushoto wa Manchester City, Benjamin Mendy mwenye umri wa miaka 26, anatajwa kuwa kwenye orodha ya nyota wanaotakiwa na Inter Milan. **(Manchester Evening News)**

**UNITED WAMTAKA KOUNDE**

KLABU ya Manchester United itamgeukia mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, kama mbadala wa Raphael Varane mwenye miaka 28, kama watashindwa kumsajili mlinzi huyo kutoka Real Madrid. **(AS)**

**FIRPO KUTUA JUMLA LEEDS**

MLINZI wa kushoto wa Barcelona, Junior Firpo mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kukamilisha uhamisho wake wa kudumu kujiunga na Leeds United. **(The Athletic)**



# Coastal yamulika mbili za mwisho

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kukubali kipigo cha mabao 7-0 katika mechi ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Simba, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema maandalizi ya timu yake kuelekea mechi zilizobaki yapo vizuri na wanaamini watapata matokeo chanya.

Coastal Union ambayo inashika nafasi ya pili kutoka mkiani mwa ligi hiyo yenye timu 18, ikiwa na pointi 34 baada ya kushuka dimbani mara 32, Jumamosi wiki hii itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 73 ilizokusanya kutokana na mechi 30, itaikaribisha Coastal Jumamosi ikitaka kuendeleza maumivu iliyoyatoa katika mechi ya mzunguko wa kwanza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kwa kuichapa 7-0, mchezo ambao John Bocco alipiga hat-trick.

Akizungumza na mwandishi wetu, Mgunda ambaye timu yake baada ya mchezo huo itahitimisha msimu kwa kuikaribisha Mwadui FC kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, alisema ushindani ni mkubwa na kila timu inahitaji ushindi hivyo vijana wake watafanya vizuri.

"Kikosi kipo vizuri, kila mchezaji anajua kwamba tunahitaji ushindi na mechi zetu ambazo zimebaki ni lazima tupambane, hivyo mashabiki waendelee kutupa sapoti," alisema Mgunda.

Uwezekano wa Coastal Union kujinasua katika timu nne zitakazoshuka daraja moja kwa moja msimu huu ni mdogo sana na hata kupata nafasi ya kucheza mechi ya mchujo pia ni mdogo.

Msimu huu timu nne kutoka mkiani, zitashuka daraja moja kwa moja huku zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kwenye msimamo, zikicheza mechi za mchujo dhidi ya timu zilizomaliza nafasi ya pili kutoka Kundi A na B kwenye Ligi Daraja la Kwanza ili kuwania nafasi mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Aidha, timu zilizomaliza nafasi ya kwanza kutoka Kundi A na B kwenye Ligi Daraja la Kwanza, zenyewe zimepanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo msimu ujao itashirikisha timu 16 kutoka 18 za msimu huu.



# ZULU AAHIDI KUPIKA NA KUFUNGA MENGI AZAM

**Na Saada Akida**

NYOTA mpya wa Azam FC, Mzambia Charles Zulu, amesema atapambana kumaliza kiu ya timu yake hiyo kwa kufunga na kutengeneza nafasi za mabao ndani ya kikosi hicho kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine itakayokuwa mbele yao. Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Zulu alisema anafurahi kufanya kazi na Azam FC, hivyo atahakikisha anashirikiana vema na wachezaji wenzake kufikia malengo ya timu hiyo.

Alisema hatawaangusha viongozi wa Azam FC na kocha wao, George Lwandamina, aliyependekeza kusajiliwa kwake katika kikosi cha timu hiyo kutokana na uwezo wake.

"Nafurahi kufanya kazi Azam FC, ni timu kubwa sana hapa nchini, hata Afrika Mashariki na Kati nina imani nikiwa hapa nitafanikisha malengo yangu ya kufunga na kutengeneza nafasi za mabao kwa wenzangu," alisema Zulu.

**Alisema atahakikisha anajituma na kujitoa ndani ya uwanja kuonyesha kiwango kizuri na kutowaangusha viongozi waliomsajili.**

"Kikubwa ni ushirikiano mzuri nitakaoupata kutoka kwa wachezaji wenzangu ili kufikia malengo ambayo yanatarajiwa na kila mmoja wetu," alisema kiungo huyo mshambuliaji kutoka Klabu ya Cape Town City ya Afrika Kusini.

Zulu anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, juzi alifanyiwa vipimo na kufuzu kisha kutia saini mkataba wa miaka miwili ndani ya viunga vya Azam Complex.

Azam FC imemalizana na nyota huyo baada ya kufikia makubaliano na timu ya Cape Town City aliyokuwa akiitumikia akitokea Zanaco FC ya Zambia.




Kiungo mshambuliaji mpya wa Azam FC, Mzambia Charles Zulu (kushoto), akisaini mkataba mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' juzi. **PICHA: AZAM**

# Polisi Tanzania wataka tano bora

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikiwa imebakiza mechi mbili za nyumbani kabla ya msimu kumalizika, uongozi wa Polisi Tanzania umeweka wazi nia yao ya kufikia malengo ya kumaliza nafasi tano za juu msimu huu.

Polisi Tanzania ambayo imebakiza mechi dhidi ya Kagera Sugar na Mwadui FC, kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, kwa sasa ipo nafasi ya saba ikiwa na pointi 42 sawa na KMC FC iliyopo nafasi ya sita, lakini ikiwa nyuma mechi moja kutokana na kushuka dimbani mara 31.

Katika nafasi ya tano ipo Namungo FC yenye pointi 43 huku Biashara United ikiwa nafasi ya nne na alama zake 49 baada ya kushuka dimbani mara 32.

Akizungumza na mwandishi wetu, Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Hassan Juma, alisema licha ya kila timu kuwa na mipango ya kufanya vizuri, lakini na wao wanahitaji kutimiza malengo yao.

"Tunataka kuona timu inatimiza malengo yetu ya kumaliza ndani ya tano bora, na kila mchezaji anapenda kuona timu ikishinda hususan mechi ambazo zimebaki.

"Mashabiki waendelee kutupa sapoti kama ambavyo wamekuwa wakifanya, hivyo kwenye mechi ambazo tumekuwa tukicheza hilo ni faraja kwetu na kila kitu kinawezekana," alisema.

Polisi Tanzania itaikaribisha Kagera Sugar Julai 14, mwaka huu kabla ya siku nne baadaye kuhitimisha ligi hiyo kwa kualika Mwadui FC ambayo imekuwa ya kwanza kushuka daraja msimu huu.

# Michezo

Jumanne Julai 6, 2021

Nipashe




KISASI ITALIA VS HISPANIA NUSU FAINALI EURO 2020 HABARI UK 22

PASUA...



Mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, akipasua katikati ya mabeki wa Ecuador kwenye mechi ya Copa America iliyopigwa Uwanja wa Estadio Olimpico Pedro Ludovin, Brazil juzi na timu yao kushinda 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga: FA Cup tutaipiga Simba kwenye mshono

## ●●● Lakini Nabi aonya akieleza haitakuwa rahisi Wekundu hao kukubali kutobolewa tena baada...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela akiwatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuelekea kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu Kombe la FA kuwa wanakwenda kulichukua kombe hilo dhidi ya Simba, Ofisa Mhamasishaji wa klabu hiyo, Antonio Nugas amesema "tutaipiga kwenye mshono".

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mwakalebela amesema baada ya kuwanyoa Simba bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kilichobaki ni kwenda kulitwaa Kombe la FA kwa kuichapa katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

"Tunawaambia Simba kuwa sisi tunatangulia Kigoma, watatukuta," alisema kiongozi huyo.

Alisema ushindi wa Jumamosi aliutarajia kutokana na maandalizi waliyoyafanya, huku akimwagia sifa Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi.

'Ni 'dabi' yake ya kwanza, lakini kocha ameanza kwa mguu mzuri, ameona vitu vingi na amejifunza vitu vingi kwa hiyo tunategemea hata kwenye mechi ya Kigoma tutafanya vizuri. Lengo letu ni makombe matatu msimu huu, tayari moja la Mapinduzi, na la pili linaweza likawa ndiyo hilo la FA tutakalokwenda kuchukua. Nilikuwa na imani sana na kikosi cha Yanga kwa sababu kinaweza kukupa ushindi wakati wowote na wamedhihirisha hivyo. Niwapongeze pia vijana wangu," alisema Mwakalebela.

Kiongozi huyo amewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuwa na imani na viongozi wao waliopewa dhamana ya kuiongoza klabu yao na kuwakabidhi timu ili wawe na furaha.

Kwa upande wa Nugas, alisema kikosi cha Yanga kwa sasa kimezidi kuimarika chini ya Nabi na hana wasiwasi kuhusu mechi hiyo ya fainali kwa sababu wanakwenda kutonesha kidonda cha Simba kwa kupiga kwenye mshono.

"Sisi huwa hatuongei sana, walisema wachezaji wetu ni wakuokoteza, na wakalisikia hilo kwa kuwaonyesha kuwa wao ni bora, hivyo sasa tunakwenda Kigoma kupiga tena kwenye mshono," alisema.

Lakini Kocha Mkuu, Nabi yeye amewataka wachezaji wake wasibweteke na kusahau kwamba wana dakika 90 zingine dhidi ya Simba katika fainali ya Kombe la FA.

Nabi aliliambia Nipashe jana kuwa wanafurahi kupata ushindi dhidi ya watani wao, Simba, lakini bado wanakibarua kigumu katika mchezo huo wa fainali.

Alisema Simba hawatakubali kufungwa kwa mara nyingine, jambo ambalo anaamini watakuingia kwa mbinu zingine kuhakikisha wanalipa kisasi katika mchezo huo.

"Tutasherehekea, tutafurahi kuifunga Simba, ila wachezaji wanatakiwa kutambua tunakutana nao tena katika fainali, hawatakubali kufungwa na watakuja na hasira na kutaka kulipa kisasi.

"Kila mechi kwetu ni muhimu. Fainali ni muhimu sana kwa sababu tunahitaji kutwaa kombe hilo, lazima tupambane na tusilewe sifa za kushinda mechi hiyo wakati kuna mchezo mgumu mwingine," alisema Nabi.

Timu hizo zitashuka katika Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma Julai 25, katika mechi hiyo ya fainali, ambayo Simba itakuwa ikitetea taji hilo baada ya kulitwaa mwaka jana kwa kuifunga Namungo FC.

## WACHEZAJI WASHIKILIA KIBARUA CHA MANARA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia timu yao ikikubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, ametangaza kuachia ngazi endapo watafungwa tena katika mechi ya fainali ya Kombe Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu Kombe la FA.

Simba ambayo ilikuwa inapewa nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi katika mchezo huo uliopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilijikuta ikiambulia kipigo hicho, shukrani kwa Zawadi Mauya aliyepeleka kilio hicho Msimbazi.

Lakini, Simba ina nafasi ya kulipa kipigo hicho, timu hizo zitakapokutana Julai 25, mwaka huu katika Uwanja wa Lake Tanganyika kwenye mechi ya fainali ya FA Cup.

Kuelekea mchezo huo, Manara amemwambia nahodha wa timu hiyo, John Bocco: "Sema na wenzio broo...mtakuja kuua watu kwa makundi siku moja, naambiwa Dar kuna shabiki kajipiga kitanzi huko, 'half' (kipindi) ya kwanza mmecheza kama mmelazimishwa au mnadai kitu, mmezinduka 'second half' (kipindi cha pili) na wao wakaweka contena mechi ikaisha.

**"Wallah Kigoma tukifungwa naacha hii kazi narudi shamba kulima, viongozi wanatimiza majukumu yao, mashabiki wanajaa kuliko mashabiki wao kwa mbali mno, mimi natukanwa kutwa kwa kuwapa nguvu nyie, lakini mmeenda kutuangusha.**

"Sioni sababu ya kuendelea na kazi hii kama wachezaji hawajui nini maana ya uzito wa 'derby' (dabi), wachezaji wao wanajitoa asilimia elfu moja kutoka dakika ya kwanza, sisi tunazinduka kushakuchwa, kaeni wenyewe zungumzeni na thamani ya jezi ya @simbasctanzania ilindwe."


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002